SUPA JACKPOT
TZS. 1,027,393,141
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 4

**ADAI** jina tata limemweka selo siku 60, hukumu yake yakwama




UKURASA 11

# Nipashe

Alhamisi Septemba 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581055

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Abiria, wadau wapinga uamuzi stendi Magufuli

**WAZIRI** akiri shida, ataka hatua...*Endelea ukurasa wa 2*



Waziri wa TAMISEMI, Innocent Bashungwa

## Mbowe: Tozo benki ni kodi mara mbili kwa watumishi

UKURASA 2


UKURASA WA 5

### DED ASIMAMISHWA KAZI SIKU 19 BAADA YA ONYO

SIKU 19 baada ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kutoa onyo kwa viongozi wa serikali Wilaya ya Muheza, kuacha misuguano...

## Agizo la Rais ubambikaji kesi lawaibua watetezi

UKURASA 3




Waziri wa Maendeleo ya Jamii Zanzibar, Riziki Pembe Juma (wa tatu kushoto), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 2.5 kwa Khatib Haji Hamis (wapili kushoto), baada ya kuibuka mshindi wa jumla katika mashindano ya 'CRDB Bank Ngalawa Race', yaliyoandaliwa na benki hiyo katika Tamasha la Kizimkazi, kwenye fukwe za Kizimkazi Mkunguni, Mkoa wa Kusini Unguja, Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

MICHEZO JOTO LA NAMBA LATIKISA SIMBA UK.24 KABWELA UK.18



Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Baraza la Mawaziri, Ikulu, Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Abiria, wadau wapinga uamuzi stendi Magufuli

**Na Waandishi Wetu**

ABIRIA na wadau wakuu wa Stendi Kuu ya Magufuli ya mabasi yaendayo mikoani iliyoko Mbezi mkoani Dar es Salaam, wamelalamikia utaratibu uliosheheni adha kwa abiria wanaoingia na kutoka.

Ni hatua inayokuja siku moja baada ya kuwapo abiria waliogoma kushuka kwenye mabasi, walipotakiwa kufuata utaratibu mpya uliowekwa wa abiria wote kushuka kwenye stendi hiyo hata kama basi walilopanda linakwenda mjini. Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya abiria walilalamikia utaratibu huo unawaongezea gharama kwa sababu wanapotaka kusafiri hulazimika kuchukua usafiri mwingine wa pikipiki, bajaji au taxi kuwahi stendi baada ya kampuni za mabasi hayo kutoruhusiwa kuchukua abiria kutoka kwenye ofisi zao.

Mkazi wa Bunju, mkoani Dar es Salaam, Anna Peter, alisema alisafiri juzi kutoka Kigoma na kuwasili Stendi ya Magufuli saa 10 alfajiri na basi lilipoingia kituoni walitangaziwa abiria wote kushuka.

Alisema wakati wakiwa safarini kondakta aliwatangazia basi litakaposhusha abiria Stendi ya Magufuli, litaelekea Ilala na kuwataka wanaolekea maeneo hayo wabaki ili washushwe kwenye vituo vyao. "Cha kushangaza baada ya kondakta kushusha mizigo ya abiria waliokuwa wameteremkia Stendi ya Magufuli, alikuja ndani ya basi na kututangazia utaratibu mpya unaotaka abiria wote washushwe hapo na basi liondoke bila abiria," alisema. Tangazo hilo lilikuwa changamoto kwa abiria kwa sababu wakati huo kulikuwa hakujapambazuka na tayari wengine walikuwa wameshawasiliana na ndugu wawapokee Ubungo.

Wakizungumza na kituo cha ITV juzi, baadhi ya abiria waliokuwa ndani ya mabasi baada ya kugomea utaratibu huo, walihoji serikali inapata hasara gani kama mwenye gari ameamua kutoa msaada kuwasogeza abiria wake kituo kingine.

"Sisi tunaishi Mbagala, gari linaelekea Mbagala inapungua wapi tukifikishwa Mbagala," mmoja wa abiria alihoji. Mwingine aliyejitambulisha kwa jina moja la Focus, alihoji kama tajiri akitoa msaada kwa abiria wa kuwashusha kituo kingine na kuwaepushia adhabu ya maisha serikali inapungukiwa na nini. Meneja wa mabasi ya Dar Lux aliyejitambulisha kwa jina moja Ally, aliiomba LATRA (Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini), iruhusu utaratibu ambao ulikuwa unatumika badala ya kuwabana abiria na kuwasababishia usumbufu.

Mwakilishi wa kampuni ya mabasi ya Frester, Ezekieli Urio alidai kuwa abiria wengi wakiambiwa kituo cha kupandia basi ni Mbezi hushindwa kuelewa wapi yalikoegeshwa kwa sababu kwa siku mabasi yanayoingia huwa zaidi ya 200 na maegesho 108.

Meneja wa mabasi ya Kilimanjaro Express ambaye hakutaka jina lake liandikwe gazetini, alisema LATRA ilitoa vibali vya kujenga stendi ili kupunguza mkusanyiko mkubwa wa abiria stendi na kuhoji sababu ya kubadilisha utaratibu.

**KAULI YA SERIKALI**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, amemuagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, kukutana na wadau na wamiliki wa mabasi kuweka utaratibu mzuri ambao utakuwa shirikishi.

"Nimesikia malalamiko kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kama mchakato huu ungekuwa shirikishi basi kusingekuwa na kelele, ninamwelekeza Mkuu wa Mkoa (Amos Makalla) kuhakikisha utaratibu huu wa kutumia Stendi ya Magufuli unakuwa shirikishi. Aidha, Waziri Bashungwa alisema zipo baadhi ya sekta binafsi zimeshajenga stendi zao kwa utarabu uliotolewa na LATRA.

"Mkuu wa mkoa akae na wadau ambao wanategemea riziki kwenye stendi ya Magufuli pamoja na LATRA na kuwa na utaratibu wa kuhakikisha wanaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

"Kwa wale ambao watahitaji kupita Stendi ya Magufuli lakini wanahitaji basi hilo hilo liwafikishe mjini kwa utaratibu ambao tayari umeshakuwapo kupitia vituo vya mabasi ambavyo tayari vimeshajengwa na sekta binafsi, Mkuu wa Mkoa akae nao aangalie utaratibu mzuri."

Aliagiza uangaliwe utaratibu mzuri ambao utahakikisha sababu za kiusalama za kupita Stendi ya Magufuli na ajira zilizotengenezwa kituoni hapo zinalindwa bila kuathiri huduma bora na adha ambayo wananchi wanapata.

Alisema kwa maelekezo aliyompatia Mkuu wa Mkoa anaamini watatimiza lengo la kutumia Stendi ya Magufuli bila kuwapa adha wananchi ambao wanalazimika washukie stendi na kuingia gharama nyingine za usafiri wakati yapo mabasi yanapita hapo na kuwasogeza karibu na Jiji kama ilivyokuwa awali.

**LATRA-CCC YATETEA ABIRIA**

Kaimu Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA-CCC), Leo Ngowi, akizungumza na waandishi wa habari jana aliomba serikali kuruhusu abiria kutumia huduma zilizopo.

"Baraza linatambua uwekezaji mkubwa unaofanywa na serikali kwenye miundombinu, ikiwamo stendi hii ya Magufuli. Ni ukweli kuwa, wamiliki wa vyombo vya usafiri pamoja na abiria tunahitaji vituo vikubwa vyenye miundombinu ya kutosha kwa ajili ya usalama na kukidhi mahitaji mbalimbali ya kijamii," alisema.

Ngowi alisema Baraza limeona umuhimu wa serikali, kwa kutumia Sheria za Serikali za Mitaa na Mipango Miji ya mwaka 1982 na sheria ya Mamlaka nyingine kuweka utaratibu mzuri.

Alitaja sheria nyingine ni kama za LATRA ambazo Baraza linataka zitumike kuweka utaratibu wa kufaa wa kuwa na vituo vyenye sifa ili kuendana na mahitaji ya watumiaji na haki ya msingi ya usalama wa abiria, muda na gharama za safari. "Hii itaondoa mvutano kati ya abiria na wasimamizi wa sheria. Baraza linaiomba serikali iendelee kuruhusu abiria kutumia huduma zilizopo, wakati ikijipanga na kuweka utaratibu wa kumsaidia abiria kupata huduma bora, salama, kwa wakati na kwa gharama nafuu," alisema.

Ngowi alisema wanaona ongezeko kubwa la watu kwenye miji mikubwa lisiloendana na vituo vya mabasi vya kukidhi mahitaji ya abiria kwenye mikoa mbalimbali ukiwamo Mkoa wa Dar es Salaam.

**■Imeandikwa na Romana Mallya, Owen Bariki TUDARCo na Evence Evarist (DSJ).**

# Asilimia 99.9 wafikiwa sensa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu imesema hadi jana watu waliohesabiwa wamefikia asilimia 99.93, huku majengo 6,351,927 yakiwa yamehesabiwa katika sensa ya majengo iliyoanza juzi.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Dk. Albina Chuwa, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu maendeleo ya sensa ya watu na makazi, sensa ya majengo na sensa ya anwani za makazi.

Alisema asilimia 0.07 ya kaya zote nchini bado zitaendelea kuhesabiwa kwa njia ya simu hadi Septemba 5, mwaka huu kwa utaratibu maalum ulioandaliwa wa namna ya kuzifikia kaya hizo kupitia viongozi wa mitaa na vitongoji.

Mtakwimu huyo alisema sensa ya majengo ina dodoso lenye maswali 27 kwa ajili ya kukusanya taarifa za aina na sifa ya majengo, idadi, hali ya ujenzi, jina la mmliki, upimaji na umiliki wa nyaraka za kisheria.

Alisema sensa ya majengo inalenga kuhesabu majengo milioni 12.7 nchi nzima na hadi jana wamefikia nusu ya malengo hayo.

Alibainisha kuwa sensa hiyo itasaidia kuboresha sera mbalimbali.

Akizungumzia kuhusu bajeti ya sensa ya mwaka huu iliyopitishwa na Bunge, Dk. Chuwa alisema Sh. bilioni 400 sawa na wastani wa Sh. 6,265 kwa mtu mmoja ndiyo iliyoidhinishwa kutumika.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa mkataba wa ajira za muda kwa ajili ya kazi za sensa hiyo baina ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na makarani au wasimamizi wa sensa ambao ulianza Agosti 21, mwaka huu mwisho wake ni Septemba mosi na kusisitiza haujabadilika.

Aliomba wananchi iwapo kuna mtu au jengo halijahesabiwa wawasiliane na viongozi wa serikali na mitaa, kijiji au kitongoji cha eneo lake kwa kupiga simu namba zilizotolewa ili utaratibu wakukusanya taarifa hizo

# Mbowe: Tozo benki ni kodi mara mbili kwa watumishi

**Na Mary Geofrey**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema hakuna haja Watanzania kuwa woga kuzungumzia alichokita serikali kuwakata kodi watumishi mara mbili.

Amesema mtumishi anakatwa kodi ya mapato kupitia mshahara wake (PAYE) na baada ya kupeleka akiba yake benki, inakatwa tena licha ya kuwa fedha hizo hazikidhi mahitaji ya familia.

Mbowe alitoa kauli hiyo juzi mkoani Arusha wakati wa misa maalum ya kumbukizi ya mwaka mmoja wa kifo cha mmoja wa wanafamilia wa wanachama wa CHADEMA.

"Nchi hii inaharibika kwa sababu ya watu walio waoga, tunapowapa watawala nafasi ya kutuongoza maisha yetu na wanaamua bila kujali maumivu yanayotupata, hatupaswi kuwa waoga.

"Wengine tumechagua njia ngumu na ngumu kweli na tupo tayari kuendelea na ugumu huo. 'This is double taxion' (hii ni kutoza kodi mara mbili), pengine huwa ninakwazika sana kwa kazi ninayofanya na kuwaona waoga halafu mnalalamika huku uani na wanaowatoza kodi hiyo wanakwenda kununua V8 ya Sh. milioni 450 hadi 500," alisema.

Mbowe alisema hakuna Mtanzania anayemudu gharama za kununua magari hayo lakini kwa kuwa kuna fedha za Watanzania, wanaweza kununua na kugawa kwa viongozi mbalimbali kama mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya, mkurugenzi na jaji kila mmoja.

Aliendelea kusema kuwa, wafanyabiashara wengi hawawezi kuendesha magari mapya bali ni viongozi wa serikali pekee.

"The moment' (wakati) mnaendelea kukaa kimya, mambo haya ndiyo yanaendelea, kama tunataka mabadiliko nchi hii lazima tuache woga," alisema. Mbowe alisema viongozi wa dini wanatakiwa kuongea na hata yeye alimzungumza na Rais Samia Suluhu Hassan, akisisitiza suala la kuhubiri amani ni kupoteza muda kama hakuna haki kwa wananchi. Mbowe pia alizungumzia Uchaguzi Mkuu wa Kenya, akisema Watanzania waliangalia na kutamani walichokiona huko kwa sababu ulikuwa wa wazi.

Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, wiki iliyopita aliahidi serikali itatoa ufafanuzi kuhusu tozo mpya za benki zinazolalamikiwa na baadhi ya wadau.

## HABARI KITAIFA

# Maagizo ya Samia ubambikaji wa kesi yaibua watetezi haki

**Na Elizabeth Zaya**

WATETEZI wa haki za binadamu wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa maagizo yake kwa vyombo vya ulinzi na usalama kupunguza kesi za kubambikiwa wananchi, huku wakishauri marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kusimamia maagizo yake na kuondoa kero kwa wananchi.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, wadau hao walisema ili maagizo yanayotolewa na kiongozi huyo yatekelezwe ipo haja ya kurekebisha mfumo mzima wa kisheria.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema pamoja na kufanyiwa marekebisho mfumo wa sheria, pia alipendekeza mfumo unaoongoza Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku urekebishwe.

"Kauli ya Rais inatufurahisha sana sisi kama wanasheria na watetezi wa haki za binadamu. Kwanza, Rais ameonyesha namna asivyopendezwa na vitendo hivyo vya wananchi kubambikwa kesi, lakini pia anaonyesha namna anavyoelewa masuala ya kijinai. Kilichobaki ni kufanyia marekebisho ya kisheria ya kijinai.

"Lakini pia ifanyiwe marekebisho Police General Orders na haya yakifanyika, yatasaidia kwa urahisi kutekeleza yale anayoagiza Rais Samia pamoja na nia yake njema katika suala hili," alipongeza.

Mratibu wa Kitaifa wa Mtandao wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Ole Ngurumwa, alisema kauli ya Rais ya kutetea wananchi wanaobambikwa kesi ni ya kuungwa mkono na kuhakikisha kunafanyika maboresho katika mfumo mzima unaosimamia na kutoa haki.

"Tunampongeza sana Rais Samia kwa hatua anazochukua katika mfumo huu wa haki, lakini mwingine wa kupongezwa katika hili ni Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP). Katika kipindi hiki wameonyesha juhudi kubwa katika kushughulikia kesi za jinai na hata kuondoa wale waliobainika walibambikwa kesi, hili ni jambo jema sana.

"Tunaomba kazi hii waifanye nchi nzima, wapite kila gereza, huko nako bado kuna watu wako ndani na hawakustahili kuwa humo. Kwa mfano, kule Loliondo pamoja na kesi hizi za uchaguzi wakipita huko, watawabaini wako wengi ni muhimu wasaidiwe," alisema.

Aliomba wadau wa sheria na haki za binadamu kushirikiana kufanya marekebisho ya sheria zinazosimamia masuala hayo.

Mwanaharakati na Mchambuzi wa Siasa, Deusi Kibamba, alisema pamoja na kufanya maboresho ya kisheria, kuna haja kufanyike maboresho katika mfumo mzima wa vyombo vinavyosimamia mnyonyoro mzima wa haki.

"Na ni vyema hili nalo likaangaliwa la kupunguza muda unaotumika katika kushtaki, kufanya uchunguzi hadi kutoa hukumu. Muda unaotumika ni mwingi sana, ni vyema kabla ya kumshtaki mtu, ufanyike uchunguzi, siyo mtu anakamatwa halafu ndipo hayo mambo yanaanza kufanyika," alisema Kibamba.

Akizungumza na wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama nchini juzi mjini Moshi, Rais Samia alisema: "Nimepewa taarifa hapa kwamba kesi 1,840 zimefutwa, hazikuwa na ushahidi wa maana, polisi tu katumia nguvu yake kamata, twende peleka, na pengine ukute aliyepelekwa kakataa kutoa kitu kidogo (rushwa), bandika kosa mrundike humo.

"Au mmegongana nyumbani huko, unamtafutia angle (kona) unambambika huko, hawa ni wanadamu, hatujui wamekaa ndani muda gani, watu 1,840 serikali inalisha, jamaa zao kiguu na njia kupeleka chakula, kuhangaika, lakini wewe uliyefanya unaona raha kabisa, nimemkomesha yuko huko. Umemkomesha, wewe Mungu? Kwa hiyo hapa napo Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), nilikuona juzi ukifoka hivi, sasa ile foka iwe kwa vitendo.

"Na kikao kilichopita nilitoa maagizo, kabla ya kumpeleka mtu ndani, hakikisha umefanya kazi yako vizuri, una ushahidi wa kutosha ndipo unakwenda unamsweka ndani, lakini eti umemkamata hujapeleleza umeambiwa tu huyo msweke ndani, huo ni mzigo kwa serikali na mzigo kwa familia, sasa tuangalie vizuri haya."

Kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, polisi aliyemkamata mtuhumiwa wa uhalifu, anapaswa ama amfikishe mahakamani ndani ya saa 24 tangu alipomkamata au kumwachia huru isipokuwa kwa tuhuma zinazohusiana na adhabu ya kifo.



Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesaba za serikali (PAC), Japhet Hasunga (kushoto), akimsikiliza Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Prof. Florence Luoga, walipokutana katika vikao vya Kamati za Bunge vinavyoendelea Bungeni, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kamati ya Bunge yashtukia utendaji usioridhisha TBA

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) imeonyesha kutoridhishwa na kasi ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika utekelezaji wa majukumu yake, ukiwamo ujenzi wa nyumba za watumishi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari mara baada ya kukutana na wakala huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Jerry Silaa, alisema kamati imeona kasi ya wakala huo kutekeleza majukumu yake ni ndogo.

Silaa alibainisha kuwa wakala uliweka malengo ya kujenga nyumba za kibiashara 1,181 lakini hadi sasa zimejengwa nyumba 254, sawa na asilimia 22.

Alisema wakala una jukumu la kutoa makazi kwa watumishi wa umma na kulikuwa na lengo la kujenga nyumba 10,250 na hadi sasa zimejengwa nyumba 408 sawa na asilimia nne.

"Kasi ya wakala kukusanya madeni yanayotokana na pango la majengo yake, imekusanya kwa asilimia 37," alisema.

Silaa alisema lengo lilikuwa ni kukusanya madeni Sh. bilioni 160 lakini hadi ni sasa Sh. bilioni 60.6 zilizokusanywa.

Kuhusu hali ya majengo yanayojengwa na wakala huo, mwenyekiti huyo alisema bado hairidhishi na sura ya majengo yanayojengwa.

"Wakala unajenga majengo ya viongozi, ukiambiwa hii ni nyumba ya jaji, mkuu wa mkoa ni majengo ambayo yanafanana na ule ujenzi hauleti hadhi ya kuonyesha hapa ni kwa kiongozi, makazi wanayojenga watu binafsi na wakala hayafanani," alisema.

Silaa alisema kamati imeelekeza kuongezwa kasi ya utekelezaji wa majukumu ya wakala na kuhuwisha usanifu wa majengo yake ili sura yake iwe bora na kuwa na majengo yanayoendana na kasi ya ukuaji wa miji.

"Serikali kuhamia Dodoma tulitarajia serikali iwe inatoa makazi bora kwa watumishi ambao wamehamishiwa Dodoma. TBA ingekuwa inatekeleza majukumu yake kwa kasi, ingewapunguzia adha wanayoipata ya kutafuta makazi kwa watu binafsi, inaweza kuathiri utendaji kazi wenye tija kwa serikali," alitoa angalizo.

Kiongozi huyo wa kamati aliongeza: "Kwenye usanifu ukiangalia sura ya nyumba ikuvutie, lakini ukiangalia nyumba zote zinafanana, yaani tumeshindwa kuwa wabunifu kwamba ukiangalia nyumba ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Kigoma zitofautiane, zinaweza hata kubeba desturi na tamaduni za eneo husika lakini ukiangalia nyumba zile zinafanana," alisema.

UN WOMEN

**DEADLINE EXTENDED – CALL FOR PROPOSALS**

The United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women (UN Women) Tanzania, under it's project on Strengthening Women's and Girls' Meaningful Participation, Leadership, and Economic Rights at Local Levels (WLER), is pleased to announce a **Call for Proposals** from organizations with a track record in human rights, women's rights and gender equality to implement creative and innovative strategies, approaches, and interventions to transform gender norms, discriminatory behaviour and practices; as well as to promote women and girls' voices, meaningful participation, leadership, and economic rights at the local level (ward, village, streets, vitongoji, e.t.c.) in the selected district councils of Dar es Salaam, Coast, Lindi, Mtwara, Arusha and Singida.

The organizations should have a base and previous experience in implementing projects in the respective regions. If it's a national organization that does not have experience in the respective regions, but plans to expand its projects to the WLER Project regions building on learnings from similar projects, it should indicate previous collaboration with other human and women's rights organizations and networks including those promoting the rights of young women and women with disabilities and duty bearers, including local government actors and community facilitators in the respective regions to deliver on the project objectives. The organizations should also demonstrate experience working with key influencers such as community and traditional leaders, religious leaders, male gender equality and women's empowerment champions, decision-makers and the media.

The full Call for Proposal (CFP) may be downloaded from:
**https://www.unwomen.org/en/about-us/programme-implementation/2022/08/call-for-proposals-unw-esa-tza-2022-001-transforming-gender-norms**

The deadline for the Call for Proposals has been extended to **16th September at 23.59** hrs (EAT) (Tanzanian Time).

**All proposal MUST be submitted through email cfp.tanzania@unwomen.org with subject line REF: CFP No. UNW-ESA-TZA-2022- 001 on Transforming Gender norms and discriminatory behaviours and practices at local levels to promote women and girls' voices, meaningful participation, and leadership.**

Only those short-listed will be contacted for further screening and consideration.

**Proposals received after the deadline will not be considered.**

For more information, please email: **agness.hanti@unwomen.org** by **16th September 2022 at 23.59 hrs (EAT).**

217023402

# Adai utata jina umemweka mahabusu siku 60, hakimu akwama kumhukumu

**Na Grace Gurisha**

MSHTAKIWA Mzawad Katebaro ameieleza Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwamba amekaa mahabusu siku 60 katika Kituo cha Polisi Chang'ombe kutokana na kufananishwa jina la mtu mwingine.

Ni hatua iliyoleta utata, hata hakimu anayesikiliza kesi hiyo, Richard Kabate, akalazimika kuahirisha kutoa hukumu aliyotarajiwa kuitoa, akisema naye uhakika wake umemwacha njiapanda.

Katebaro, anayetuhumiwa kuiba gari, alidai jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate wa mahakama hiyo kuwa jina lake ni Mzawad Katabaro na sio Katebaro kama lilivyotamkwa na upande wa mashtaka.

Wakili wa Serikali Ashura Mzava, alidai mshtakiwa amefikishwa mahakamani hapo kwa ajili ya kusomewa hukumu kwa kuwa siku ya hukumu yake ikisomwa hakuwapo mahakamani.

"Nimekaa mahabusu siku 60 katika Kituo cha Polisi Chang'ombe, siku zote hizo nawapigia kelele kwamba waniachie au wanipe dhamana kwa sababu mashtaka yaliyoandikwa yanadhaminika, lakini hawakufanya hivyo," alidai.

"Leo (jana) wananiambia nije mahakamani kwa sababu nina kifungo cha miaka mitatu jela, sielewi hakimu," alidai Katebaro.

Baada ya madai hayo, Hakimu Kabate alimtaka ataje majina yake na kutaja kuwa ni Mzawad Katabaro, pia alimtaka Wakili wa Serikali, Ashura Mzava, ataje jina la mshtakiwa huyo akadai anaitwa Mzawad Katebaro.

Kutokana na utofauti huo wa majina, Hakimu Kabate alisema anaweza akafungwa mtu ambaye hahusiki na kutoa siku 14 kwa upande wa mashtaka wamuandalie ripoti ili wajue watafanyaje Septemba 19, 2022.

Pia, Hakimu Kabate alimueleza mshtakiwa kwamba hawezi kuandika chochote alichokidai kwa sababu hajui mbele yake yuko nani, hukumu iliyotolewa Novemba 8, 2021 ina jina tofauti na analolitaja mshtakiwa.

Kabate alisema, hawezi kusema mshtakiwa arudishwe wapi kwa sababu hajui alipotokea, lakini anataka upande wa mashtaka siku hiyo umlete mahakamani.

Katebaro alihukumiwa kifungo cha miaka mitatu gerezani, baada ya kupatikana na hatia ya wizi wa gari na kukutwa na mali inayodhaniwa kwamba ni ya wizi.

Mshtakiwa huyo, anatuhumiwa kuruka dhamana na kusababisha kesi hiyo isikilizwe upande mmoja na kutolewa hukumu.

Inadaiwa, Desemba 3, 2019 mshtakiwa akiwa mtaa wa Mwinyitanga, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam aliiba gari aina ya Toyota Porte yenye thamani ya Sh. milioni 12.5.

Pia, inadaiwa Januari 12,2021 akiwa eneo la Manyovu Buhingwe, Kigoma alikutwa na gari hilo linalodhaniwa kuwa ni la wizi.



Meneja wa Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Mkoa wa Tanga, Upendo Lugongo (kushoto), akizungumza na Mkandarasi anayejenga mradi wa maji, Kata ya Mkalamo, wilayani Pangani juzi, ambapo alimtaka kukamilisha mradi huo kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Mtoto wa Mwinyi azikwa kijijini kwake

**Na Mwandishi Wetu**

Mamia ya wananchi wakiwamo viongozi wakuu wa serikali wamehudhuria maziko ya mtoto wa pili wa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano, Ali Hassan Mwinyi, Hassan Ali Hassan Mwinyi (70), yaliyofanyika kijijini Mangapwani, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Hassan aliwahi kuwa mtumishi mstaafu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Muungano na kushika nyadhifa mbalimbali. Alifariki dunia juzi katika Hospitali ya Mnazi mmoja baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Mtoto wa kwanza wa Rais mstaafu Mwinyi, Asha Ali Hassan Mwinyi, alisema kaka yake alikuwa miongoni mwa watoto 12 ambaye katika uhai aliwahi kuwa Ofisa Mwandamizi wa Shirika la Meli la Zanzibar pamoja na Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje, Zanzibar.

Asha alisema alipostaafu utumishi wa serikali alijishughulisha na shughuli zake binafsi za biashara za aina mbalimbali nchini.

Maziko yalihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiongozwa na Mzee Mwinyi, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi, marais wastaafu wa Zanzibar akiwamo Dk. Abeid Amani Karume, Dk. Ali Mohamed Shein pamoja na Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano, Mizengo Pinda.

# Mashahidi 24 kutinga kortini dhidi ya Kisena

**Na Grace Gurisha**

VIELELEZO 60 na mashahidi 24 kutolewa ushahidi dhidi ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Mradi wa Usafirishaji wa Mabasi yaendayo haraka (UDART), Robert Kisena na wenzake watatu wanaotuhumiwa kuhujumu uchumi katika Mahakama Kuu, Devisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi 'Mafisadi'.

Washitakiwa wengine katika kesi hiyo ni Charles Newe, ambaye pia ni Mkurugenzi wa UDA, na UDART, John Samangu, mfanyabiashara na Tumaini Kulwa ambaye ni mtunza fedha wa UDART.

Mahakama hiyo ilifikia hatua hiyo jana, baada ya washtakiwa kusomewa mashtaka yao upya, idadi ya mashahidi pamoja na vielelezo mbele ya Jaji Elinaza Luvanda.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili wa Serikali Timotheo Mmari, akisaidiana na Wakili Tumaini Mafuru, alidai washitakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 15 yakiwamo kuisababishia UDART hasara ya Sh. milioni 750.

Pia, wanatuhumiwa kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji fedha, kuwasilisha nyaraka za uongo na kughushi.

Washtakiwa hao wanadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Mei 25 na Julai 10, 2016 maeneo tofauti jijini Dar es Salaam.

Wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu na kujipatia Sh. milioni 750 kutoka akaunti ya UDART iliyopo katika benki la NMB tawi la Bank House.

Katika mashtaka ya kughushi, Kisena, Newe na Kulwa wanadaiwa Mei 26, 2016 jijini Dar es Salaam, kwa udanganyifu walighushi fomu 'fund transfer request' wakijaribu kuonesha UDART, imehamisha kiasi hicho cha fedha kutoka akaunti yake iliyoko benki ya NMB kwenda akaunti inayomilikiwa na Kampuni ya Long Way Engineering Ltd, iliyoko benki ya KCB, kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya mabasi na uzio eneo la Kimara, Kivukoni, Ubungo na Morocco, wakati wakijua sio kweli.

Baada ya kusomewa mashtaka hayo, washtakiwa walikana kutenda makosa hayo na waliposomewa hoja za awali walikiri taarifa zao binafsi.

Kwa upande wa Kisena alikubali majina yake na vyeo vya Mkurugenzi wa UDART, Mkurugenzi wa Kampuni ya Zenon Oil, and Gas na Mkurugenzi wa Simon Group.

Mshtakiwa Newe, alikubali majina yake na cheo cha Mkurugenzi wa UDA - Rapid, Shirika la usafiri Dar es Salaam na mshtakiwa Samangu, alikubali majina yake na pia alikiri kuwa ni mtia saini katika Kampuni ya Oil and Gas na Kulwa alikiri majina na mwajiriwa wa UDART ambaye ni mtunza fedha

Baada ya maelezo hayo upande wa utetezi ambao ulikuwa na mawakili wanne wakiongozwa na Nduruma Majengo, waliomba kupewa muda wa kuwasilisha idadi ya mashahidi na vielelezo.

Jaji Luvanda, alikubaliana na ombi hilo na kuwataka kuwasilisha mahakamani hapo idadi hiyo Septemba 9, 2022. Washtakiwa walirudishwa rumande hadi siku ya kuanza kusikilizwa mashahidi upande wa mashtaka Oktoba 7, mwaka huu.

HABARI KITAIFA




Msemaji wa Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii wa Chama cha ACT-Wazalendo, Mwanaisha Mndeme, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, wakati akitoa ushauri kwa serikali kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) katika kuboresha utoaji huduma baada ya kuelemewa na madeni ya matibabu kwa wanachama wake. **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# ACT-Wazalendo yapendekeza mifuko ya jamii kuunganishwa

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimeishauri serikali kuunganisha mifuko ya hifadhi ya jamii na bima ya afya ili kila Mtanzania apate huduma ya matibabu kupitia bima ya afya kwa wote.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Msemaji wa Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii wa ACT-Wazalendo, Mwanaisha Mndeme, alisema sehemu kubwa ya Watanzania wamejiajiri kwenye sekta isiyo rasmi ambayo inachukua asilimia 52 ya nguvu kazi yote nchini na kushauri waunganishwe na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ili kupanua fao la matibabu.

Alisema watu walio katika ajira rasmi kwenye sekta ya umma na binafsi ni watu milioni 3.5 sawa na asilimia 14.2 pekee, na kwamba watu wote wasiokuwa kwenye ajira rasmi hawana mfumo mzuri wa matibabu, pensheni, likizo au mapumziko ya uzazi wala kulindwa na majanga.

"Tunapaswa kuunganisha mfumo wa hifadhi ya jamii kwa kila Mtanzania ili anapochangia hifadhi ya jamii awe anapata huduma ya afya moja kwa moja na tunashauri serikali ihakikishe kila Mtanzania anakuwa kwenye mfumo wa hifadhi ya jamii ili kuwawezesha wananchi wote kupata bima ya afya ya taifa," alisema Mwanaisha.

Vile vile, alisema kwa mujibu wa ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya 2020/21, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wa (NHIF) kwa sasa unaendelea kuendeshwa kwa hasara na kwa mwaka huo ulipata hasara ya Sh. bilioni 109.71.

Akifafanua kuhusu ripoti hiyo, alisema udhaifu wa kiutendaji wa NHIF ambao ulisababisha hasara ya fedha nyingi, ulitokana na ukusanyaji hafifu wa madeni, utoaji mikopo na uwekezaji mbovu wa fedha za umma.

Alitoa wito kwa serikali kuhakikisha mikopo inayodaiwa kupitia mashirika ya umma na wizara kurudishwa haraka ili kuupa uwezo mfuko huo wa bima ya afya kujiendesha wenyewe.

"Serikali isimamie uwekezaji unaofanywa na mfuko wa NHIF ili kuhakikisha unaleta tija katika mapato yake, ACT inaamini katika upatikanaji wa bima ya afya kwa Watanzania wote na hili ni ahadi yetu kwa wananchi wote, kuwa tutaendelea kupigania upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa wananchi wote bila kujali kipato chao," alisema Mwanaisha.

# DED asimamishwa kazi siku 19 baada ya onyo

**Na Mary Geofrey**

SIKU 19 baada ya Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, kutoa onyo kwa viongozi wa serikali Wilaya ya Muheza, kuacha misuguano, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amemsimamisha kazi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga, Nassib Bakari Mmbaga, ili kupisha uchunguzi.

Sababu za kusimamishwa kwake zimetajwa kuwa ni kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo sambamba na utendaji kazi usioridhisha.

Kabla ya hatua ya kusimamishwa kazi kwa DED huyo, Katibu Mkuu wa CCM, Chongolo, alitoa angalizo kwa mkurugenzi huyo na viongozi wengine wa wilaya hiyo, kujirekebisha ndani ya miezi mitatu kabla ya kuchukuliwa hatua kutokana na kuwapo kwa migogoro baina yao.

"Hapa pana shida, na mimi ni Katibu Mkuu wa CCM yenye serikali, siwezi kuondoka nisiseme, lakini hata nikiondoka nitaendelea kufuatilia la sivyo tutashauri vinginevyo, lazima niwe mkweli hapa mambo hayaendi kwa kasi tuliyoitegemea katika mazingira niliyoyaona," alisema Chongolo.

Alimtaja Mkuu wa Wilaya hiyo, Halima Bulembo, kusimamia na kutekeleza majukumu aliyopewa na Rais Samia Suluhu Hassan, bila kujali kimo na umri wake.

"Mbona mnakaa kienyeji hapa! Muheza naondoka, lakini niwaambie naondoka na picha mbaya ya uongozi, na mimi ni mkweli, Katibu Mkuu nisipokuwa mkweli nitaleta picha mbaya na nitakuwa siwapendi, nendeni mkakae mrekebishe mambo sawa jamani?"

"Mkurugenzi (Nassib Mmbaga) umeletwa hapa kusimamia halmashauri, kama kuna mtu aliye mrefu kuliko wewe ni huyo RAS (Katibu Tawala wa Mkoa, Pili Mnyema), kiongozi wako ni huyo mkuu wa wilaya lazima mjue hivyo," alisisitiza Chongolo.

Aliahidi kutolifumbia macho suala hilo na kulifikisha kwa Mwenyekiti wa CCM, Rais Samia, kwa uzito unaostahili ili kuwasaidia wananchi wa Muheza.

Wakati akitangaza hatua hiyo ya kumsimamisha kazi, Bashungwa alitoa tahadhari kwa wakurugenzi wa halmashuri zote nchini kuendelea kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni kwa mujibu wa taratibu za utumishi wa umma pamoja na kusimamia miradi ya maendeleo kikamilifu.

# Mashindano ya CRDB yawa kivutio cha utalii

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amesema mashindano ya 'CRDB Bank Ngalawa Race' yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB, katika Tamasha la Kizimkazi ni mfano wa michezo ya utamaduni inayotangaza utalii visiwani humo.

Riziki, alibainisha hayo juzi wakati akifungua mashindano hayo katika hafla iliyofanyika kwenye fukwe za Kizimkazi Mkunguni ambako mamia ya watu walijitokeza kushuhudia mtanange mkali wa washiriki mahiri 20 wa mchezo wa 'Resi za Ngalawa' kutoka Kizimkazi Mkunguni na Kizimkazi Dimbani.

"Ni imani yangu kuwa mchezo huu utasaidia kuongeza thamani kwa fukwe zetu kwa kutoa burudani kwa watalii wanaotembelea katika visiwa vyetu na kutoa ajira kwa vijana wetu," alisema huku akitoa changamoto kwa Wizara za Michezo na Utalii kushirikiana na Benki hiyo kuendeleza mchezo huo.

Aliishukuru Benki ya CRDB, kwa kuwa mstari wa mbele kusaidia jitihada za serikali katika kutatua shida zinazoikabili jamii na kuwaletea wananchi maendeleo.

"Niwapongeze kwa namna ambavyo mnajitoa kusaidia jamii. Ufadhili wenu katika miradi ya maendeleo hapa Kizimkazi unaonyesha kiu mliyonayo katika kuboresha maisha ya Watanzania," alisema.

Mkurugenzi wa Mawasiliano Benki ya CRDB, Tully Esther Mwambapa, alisema benki hiyo imeamua kuwekeza katika mchezo huo wa 'Resi za Ngalawa' kwa kuwa ni moja ya michezo ya asili nchini ambayo ikitangazwa vizuri inaweza kutangaza utamaduni wa Wazanzibar na kuvutia watalii kuja kutembelea nchini.

"Rais wetu, Mama Samia, amefanya jitihada kubwa katika kutangaza vivutio vya utalii nchini kupitia filamu ya 'Tanzania The Royal Tour', tukiwa benki kiongozi na ya kizalendo nchini, tumeona ni vyema kuunga mkono jitihada hizi kupitia mashindano haya ambayo asili yake ni katika visiwa hivi vya Zanzibari," alibainisha.

Alisema, lengo lingine la kuandaa mashindano hayo kwa mwaka wa pili mfululizo kupitia Tamasha la Kizimkazi kuutumia mchezo huo wa Resi za Ngalawa kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuufanya mchezo kuwa wa kibiashara kama ilivyo michezo mingine.

"Katika kutekeleza azma hii, mwaka huu tumekabidhi vifaa vipya kwa washiriki wote 20 vyenye jumla ya thamani ya Sh. milioni 50 ikiwamo ngalawa za kisasa na maboya ya uokoaji. Hii imeongeza hamasa kubwa sana kwa washiriki ambapo mashindano ya mwaka huu yamekuwa na ushindani mkubwa," alisema.

Washiriki hao 20 walishindana katika resi za maili mbili kwa mizunguko miwili ambapo Khatib Haji Hamis, mkazi wa Kizimkazi Mkunguni, aliibuka mshindi wa kwanza na kuondoka na zawadi ya Sh. milioni 2.5 na boti ya uvuvi kwa ajili ya kikundi kutoka kijiji anachotoka.

Mshindi wa pili alikuwa Juma Ramadhani Haji kutoka Kijiji cha Kizimkazi Mkunguni, ambaye aliondoka na kitita cha Sh. milioni moja, wa tatu alikuwa Muhammad Ambar Mpate kutoka Kijiji cha Kizimkazi Mkunguni ambaye alipata zawadi ya Sh. 700,000 na mshindi wa nne alikuwa Daudi Wajihi Zahor, mkazi wa Kizimkazi Dimbani ambaye alijishindia Sh. 500,000.

Mbali na mchezo wa 'Resi za Ngalawa', Benki ya CRDB pia imetumia zaidi ya Sh. milioni 65 kudhamini michezo mingine katika Tamasha la Kizimkazi ikiwamo; mpira wa miguu, mpira wa pete, nage, mbio za baiskeli, bao, kukuna nazi, kuvuta kamba na uchoraji.

Benki hiyo pia, imejenga maabara ya kisasa ya sayansi iliyokamilika pamoja na vifaa vyake katika Skuli ya Kizimkazi yenye thamani ya Sh. milioni 50. Maabara hiyo inalenga kuhamasisha wanafunzi kusoma masomo ya sanyansi.

Tamasha la Kizimkazi linatarajiwa kufikia tamati Jumamosi ya ambapo mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan. Miradi mbalimbali ya maendeleo inatarajiwa kukabidhiwa siku hiyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kilio cha wasafiri Stendi ya Magufuli kipatiwe ufumbuzi

**KILIO** kikubwa cha wasafiri wanaotumia kituo kikubwa cha mabasi yanayotoka na kuingia kutoka mikoani, Stendi ya Magufuli ni adha ya usafiri baada ya kushushwa kwenye kituo hicho.

Kubwa wanalolilalamikia ni gharama wanayoingia kutafuta usafiri wa kuwafikisha kwenye maeneo yao wanayoishi hasa wanapoingia jijini Dar es Salaam usiku mwingi.

Malalamiko kutoka kwa baadhi ya wasafiri ni kitendo cha baadhi ya kampuni za usafirishaji kuamua kuwarahisishia gharama ya usafiri abiria wao kuanzia safari kwenye ofisi za mabasi yao hadi kwenye kituo kikuu cha Mbezi.

Hata hivyo, imedaiwa kuwa kampuni hizo zimepigwa marufuku kuchukua abiria kwenye vituo vya ofisi zao na badala yake abiria wawakute kwenye kituo kikuu kilichopangwa ambacho ni Mbezi.

Maswali yanayoibuka kwa baadhi ya wadau ni kuwa kwanini basi liondoke likiwa tupu hadi Mbezi ilihali kuna abiria wanaoishi maeneo ya karibu na ofisi zao ambao wangeweza kuwasaidia kwa kuwarahishia usafiri.

Vivyo hivyo, malalamiko yamekuja kwa abiria wanaotoka mikoani kulazimika kushukia kituo cha Mbezi na kutafuta usafiri mwingine wa kuwafikisha majumbani kwao.

Kilio kinachotolewa na wananchi wengi ni muda wa baadhi ya mabasi yanayoingia kutoka mikoani kuwa ni usiku mwingi na gharama wanazoingia kupata usafiri wa kuwafikisha makwao kuwa zaidi ya mara mbili ya nauli waliyolipia tiketi. Yaani unaweza ukatoka Morogoro hadi Dar es Salaam kwa gharama ya tiketi ya Sh. 9,000, lakini usafiri wa kukutoa Mbezi hadi unapoelekea ukaambiwa ni Sh. 20,000.

Kwa kweli gharama hizo ni kubwa na kwa watu ambao hawana uwezo wa kulipa inawabidi walale stendi ili kukikucha watafute daladala.

Fikiria abiria mwenye watoto na mizigo ni usumbufu gani anaoupata? Na wengine hata kupoteza baadhi ya mizigo yao.

Ingawa kumetolewa ufafanuzi wa kuwa kuna madereva wa bodaboda, bajaji na taxi wanaoegesha kwenye kituo hicho kwa kufanya biashara ya kutegemea abiria wanaoshuka kwenye mabasi hayo, lakini ukiangalia ni abiria wachache wanaobaki kwenye mabasi yanayokwenda kupaki kwenye ofisi zake, huku wengi wakiteremkia kituo hicho.

Ni kweli wafanyabiashara wanatafuta riziki zao kupitia abiria hao, lakini watu wasilazimishwe kufuata taratibu ambazo zinawagharimu na wengine kulazimika kutofanya safari hata za kusalimia ndugu zao mikoani kwa kukwepa gharama hizo.

Kwa mfano mtu ametoka mkoani na anashukia Kimara, inamlazimu kushukia Mbezi, wakati basi alilopanda kumtoa mkoani linapita kituo hicho hicho anachoshukia. Hii haijakaa sawa.

Tunashukuru Waziri wa TAMISEMI, Innocent Bashungwa kwa kuliona hilo na kumuagiza Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla kukutana na wadau na wamiliki wa mabasi ili kuweka utaratibu mzuri na shirikishi wa utoaji huduma kwa wananchi kwenye kituo hicho kikuu cha mabasi cha Magufuli.

Waziri amesema amekuwa akifuatilia kwa ukaribu malalamiko yanayotolewa na wananchi kuhusu huduma katika stendi hiyo.

Amemtaka Mkuu wa mkoa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), pamoja na wadau wengine ili kukubaliana na kuweka utaratibu utakao rahisisha utoaji huduma bora bila kuleta adha kwa wananchi wala kuathiri malengo ya serikali kujenga stendi hiyo.

Ni matumaini yetu kuwa mazungumzo yatakwenda vizuri na kupata muafaka wa kumaliza adha hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Wazazi na walezi pelekeni watoto wenu kupata chanjo hii ya polio

**NAAM!** Ni rasmi kampeni ya siku nne ya kutoa chanjo ya matone kwa ajili ya kudhibiti ugonjwa wa polio kwa watoto wa umri chini ya miaka mitano, katika mikoa yote nchini.

Chanjo hiyo itakuwa ni ya awamu ya tatu kwa mwaka huu wa 2022 ikilenga kufikia watoto milioni 12. 3 ili kuwaepusha na ugonjwa huo unaotajwa kuathiri mfumo wa 'neva' na huweza kusababisha udhaifu wa misuli au kupooza.

Machi mwaka huu, chanjo hiyo ilitolewa mikoa minne inayopakana na nchi ya Malawi ambayo ni Mbeya, Songwe, Ruvuma na Njombe, watoto milioni 1.1 sawa na asilimia 115 wa chini ya miaka mitano walichanjwa.

Baada ya hapo, awamu ya pili ya chanjo ilitolewa nchi nzima kuanzia Mei 18 hadi 21 mwaka huu na kuwafikia watoto 12, sawa na asilimia 118.8 na leo inaanza chanjo ya awamu ya tatu.

Hapo namrejea Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu katika taarifa yake kwa umma alipokuwa akitangaza kuanza kwa kampeni hiyo, kutokana na mlipuko wa ugonjwa huo uliotokea katika nchi za jirani. Katika ufafanuzi wake ni kwamba, Februari mwaka huu nchi ya Malawi ilikumbwa na ugonjwa huo, kisha Mei mwaka huu Msumbiji nayo ikakumbwa, ambapo Tanzania imeamua kuchukua tahadhari.

Ninadhani kampeni hiyo si ya kukosa, hivyo ingekuwa ni vyema wazazi na walezi wakawapeleka watoto wao katika vituo vya kutolea chanjo hiyo kwa ajili ya kuwanusuru dhidi ya ugonjwa huo.

Ikumbukwe, wataalamu wa afya wanasema maambukizi ya polio yanaathiri mfumo wa neva na huweza kusababisha udhaifu wa misuli au kupooza, ambapo ugonjwa huo huwapata zaidi watoto wa chini ya miaka mitano.

Hivyo, ili kuwanusuru na polio watoto wa chini ya miaka mitano, njia pekee ni kuhakikisha wanapata chanjo kama ambavyo Waziri wa Afya Ummy Mwalimu amekuwa akitangazia umma wa Watanzania.

Waswahili wana msemo wao kwamba; 'ukiona mwenzio ananyolewa na wewe tia zako maji'. Majirani zetu wamekumbwa na ugonjwa huo, hivyo nasi hatuna budi kujiandaa kukabiliana nao.

Kwa kuwa inaelezwa, maambukizi ya virusi vya polio huweza kuzuiliwa kwa chanjo, hivyo ninadhani ni muhimu wazazi na walezi kufuatilia ratiba ya chanjo, ili kuhakikisha watoto wao wanapata huduma hiyo.

Ummy anakumbusha kuwa Shirika la Afya Duniani (WHO), limekuwa likielekeza kuwa unapotokea mlipuko au tishio la mlipuko wa ugonjwa, nchi yenye ugonjwa na ambayo iko jirani inapaswa kufanya kampeni ya chanjo.

Tayari kwa mwaka huu Tanzania imeshafanya awamu mbili za kampeni ya kutoa matone na chanjo na leo inaanza awamu ya tatu ambayo ninaona nikumbushe jamii kutambua umuhimu wake.

Pia muhimu wazazi na walezi wasikubali kupewa elimu potofu kuhusu chanjo hiyo kama ambavyo ilitokea kwenye chanjo ya UVIKO-19, badala yake wawapeleke watoto katika vituo vya kutolea huduma hiyo.

Kuwapo kwa kampeni ya chanjo ya polio, kumeshaelezwa kuwa ni kutokomeza na kuwakinga watoto na kuokoa gharama zinazotokana na matibabu ya ugonjwa huo, ambao inaelezwa kuwa unazuilika.

Ninagusia elimu potofu kutokana na kwamba imekuwa, ni kawaida kwa baadhi ya watu kuzusha taarifa zisizo na ukweli kwenye mambo ya msingi, hali ambayo inaweza kukwamisha huduma hiyo kwa waatoto.

Kwa mfano, baada ya ugonjwa wa UVIKO-19 kuingia nchini, kulikuwapo upotoshaji mwingi kuhusu ugonjwa huo, na hata chanjo ilipoanza kutolewa, bado kuna watu waliendelea kuipinga.

Inawezekana watu wenye mtazamo huo, wakaendesha kampeni ya kupinga chanjo ya polio na kusababisha baadhi ya wazazi na walezi wasipeleke watoto wao kupata matone ya chanjo hiyo.

Hivyo, ninadhani ni muhimu kila mzazi na mlezi kutafakari na kisha kuchukua hatua ya kumpeleka mtoto wake katika kituo cha kutolea huduma ya chanjo ya polio haraka iwezekanavyo.

# TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED

TANESCO

# TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Wananchi wote mnatangaziwa kwamba, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) litaondosha kwa njia ya mnada wa hadhara Magari, Pikipiki, Betri zilizotumika, Mafuta Machafu, Samani chakavu za Ofisi, Vifaa vya Ofisi, Vyuma Chakavu, Vifaa vya Umeme/scraps, Matairi na vifaa mbalimbali chakavu katika Mikoa na Vituo vya Kuzalisha Umeme vilivyopo Kanda ya Kusini, Kaskazini, Ziwa, Kati, Magharibi na Nyanda za juu Kusini kwa tarehe na vituo kama inavyoonekana hapo chini.

Mnada utafanywa kwa wananchi wote isipokuwa vyuma chakavu, vifaa vya kielektroniki, mafuta machafu, betri zilizotumika na matairi yaliyotumika vitauzwa kwenye makampuni yenye vibali vilivyotolewa na waziri mwenye dhamana ya mazingira kwa kuzingatia matakwa ya sheria ya mazingira ya mwaka 2004 na kanuni zake kama "Environmental Management (Control and Management of Electrical and Electronic Equipment Waste) Regulations, 2021" na "The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021"

**ORODHA YA VITUO AMBAPO MNADA UTAFANYIKA**

**KITUO NA. 1A: TANESCO SOMANGA - Tarehe 15/09/2022**
**1. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI**

**KITUO NA. 1B: TANESCO KILWA - Tarehe 15/09/2022**
**1. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KILWA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU33530 | TATA TRUCK | | MAT379040VSR24980 | 1998 |

**KITUO NA. 2: TANESCO LINDI - Tarehe 16/09/2022**
**2. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA LINDI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 39730 | ISUZU NQR 4.3 | 743177 | JAAIR66R97100012 | 2013 |
| 2 | SU 33481 | MITSUBISH PICKUP | 4D56JB451 | JMIJNK340WP003107 | 1998 |
| 3 | SU 33755 | MITSUBISH PICKUP | 4D56HQ8304 | JMIJNK340VP005724 | 1999 |
| 4 | SU 32690 | TOYOTA HILUX | 34393004 | LN1060122313 | 1996 |
| 5 | SU 34423 | FORD RANGER | 106223 | MNBBSFE801L0181799 | 2001 |
| 6 | SU 35834 | MITSUBISH L200 | | | 2003 |
| 7 | SU 35620 | TOYOTA HILUX | 3L3636811 | LN1060102119 | 2005 |
| 8 | SU 35940 | ISUZU NPR | | | 2002 |
| 9 | SU 34339 | MOTOR CYCLE SUZUKI 125 | TF125138094 | TF125137805 | 2001 |
| 10 | SU 32934 | MOTOR CYCLE YAMAHA | 3HAO33426 | 3HA033429 | 1996 |
| 11 | SU 36682 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI*0621000010* | LAELYZ4076B930026 | 2006 |
| 12 | SU 35742 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI*0221000981* | LAELYZ4073B930081 | 2003 |
| 13 | SU 36683 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM0221000875 | LAELYZ4036B930048 | 2006 |
| 14 | SU 34364 | MOTOR CYCLE SUZUKI | TF125139233 | TF138729 | 2001 |
| 15 | SU 35741 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI0221000852 | LAELYZ40X6B930001 | 2002 |
| 16 | SU 36756 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI0221000852 | LAELYZ40X6B930001 | 2006 |

**KITUO NA. 3A: - TANESCO MTWARA Tarehe 18/09/2022**
**3. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MTWARA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 35417 | MITSUBISH L200 | 4D56 | MMBJNK7403D016456 | 2003 |
| 2. | SU 39802 | ISUZU NPR | 747278 | JAANIR66P97100121 | 2009 |
| 3. | SU 31501 | TOYOTA 4C | 1HZ0100205 | HJ2800018117 | 2001 |
| 4. | SU 35807 | MITSUBISH L200 | 4D56BL4101 | MMB JNK 7404D007551 | 2003 |
| 5. | SU 36680 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0421001337* | LAELYZ 4006B930024 | 2002 |
| 6. | SU 35734 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0221000875* | LAELYZ 40X3B930074 | 2002 |
| 7. | SU 35733 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0221001015* | LAELYZ 4073B930128 | 2002 |
| 8. | SU 32933 | MOTOR CYCLE YAMAHA | 3HA033428 | 3HA033429 | 1995 |

**KITUO NA. 3B: MTWARA GAS PLANT Tarehe 18/09/2022**
**9. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI VYA MTWARA GAS PLANT**

**KITUO NA. 4: NEWALA Tarehe 20/09/2022**
**10. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA NEWALA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 39801 | ISUZU NPR | 4HF1 | JAANIR66P97100119 | 2009 |
| 2. | SU 39973 | TOYOTA HILUX | 5L6024799 | AHTFK22GX03014600 | 2006 |
| 3. | SU 34361 | MOTOR CYCLE SUZUKI | TH152FM1 8F102432 | TF 125138700 | 2000 |
| 4. | SU 35735 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0221000908* | LAELYZ4083B930073 | 2002 |

**KITUO NA. 5: MASASI Tarehe 21/09/2022**
**5. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MASASI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 39727 | ISUZU NPR | 4HF1 750295 | 97100122 | 2009 |
| 2 | SU 34360 | MOTOR CYCLESUZUKI 125 | TF 125139104 | TF 125138785 | 2000 |

**KITUO NA. 6: SONGEA MJINI Tarehe 23/09/2022**
**6. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA RUVUMA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 35736 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM10221000956 | LAELYZ 4063B930069 | 30.07.2003 |
| 2 | SU 35739 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0221000978* | LAELYZ4003B930083 | 30.07.2003 |
| 3 | SU 36678 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0621000021* | LAELYZ400XB950052 | 02.08.2006 |
| 4 | SU 35737 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM1*0221000954* | LAELYZ4003B930009 | 30.07.2003 |
| 5 | SU 34363 | MOTOR CYCLE SUZUKI | TF 125138145 | TF 125138750 | 17.05.2001 |
| 6 | SU 35943 | ISUZU NPR | 636040 | 17111135 | 2002 |
| 7 | SU 35824 | MITSUBISH L200 | 4D56 | V5M214875 | 2003 |

**KITUO NA. 7 – MOROGORO – 25/09/2022**
**7. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MOROGORO**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 33469 | MITSUBISH D/CABIN | 4D56JB6065 | JMYJNK340WP003329 | !""# |
| 2. | SU 34315 | SUZUKI MARUTI | G13BBN111422 | MG71IN0208680 | $%%! |
| 3. | SU 35808 | MITSUBISH P/UP | 4D56BL4112 | MMBJNK7404D7594 | $%%& |
| 4. | SU 35810 | MITSUBISH P/UP | 4D56BL4102 | MMBJNK7404D007683 | $%%& |
| 5. | SU 34316 | SUZUKI MARUTI | G13BBN110264 | MG71IN0208684 | $%%! |
| 6. | SU 33760 | MERCEDECE BENZ | MJ030335A101789 | ADB 3973726003375 | !""' |
| 7. | SU 29242 | HONDA | CG125E-2210654 | CG125-1623936 | |
| 8. | SU 35702 | QINGQI | 157FM10221000868 | LAFLYZ4053B930127 | |
| 9. | SU 36324 | BAJAJI | DUMBMB 18142 | DUFBMB 92745 | |
| 10. | SU 37597 | BAJAJI | DUMBRK 59426 | MD2DDDMZZRWK 03178 | $%%' |
| 11. | SU 33732 | YAMAHA 125 | 162FMJ 10062324 | L1255-5713314 | |

**KITUO NA. 8: KIDATU – Tarehe 27/09/2022**
**19. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 13 | SU 28148 | HONDA XL 125 | L125SE5531687 | L125S5420276 | 5/05/1991 |
| 14 | SU 36665 | QINGQI | 157FM10621000012 | LAELYZ4026B930039 | 2/08/2006 |
| 15 | SU 36666 | QINGQI | 157FM10621000022 | LAELYZ4006B930038 | 208/2006 |
| 16 | SU 35893 | QINGQI | 157FM10221001023 | LAELYZ4053B930144 | 12/11/2003 |
| 17 | SU 28147 | HONDA XL 125 | LI25SE551683 | L125S5420272 | 5/05/1991 |
| 18 | J1253/1 | DIESEL GENERATOR/SC 634B | STARTOR STAR,415V 3PHASE | | |
| 19 | | STANFORD GENERATOR | 700KVA/1500RPM | | |

**KITUO NA. 9 – MTERA Tarehe 29/09/2022**
**20. VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI**

**KITUO NA. 10 – DODOMA – 1/10/2022**
**21. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA DODOMA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 28375 | NISSAN DEL TRUCK | ND6084736 | UG78041426 | 13/05/1991 |
| 2. | SU 23284 | MASSEY FERGUSON | U164147P | 5103B1171 | 30/10/1991 |
| 3. | SU 34320 | SUZUKI MARUTI/STW | | | 30/04/2001 |
| 4. | SU 34314 | SUZUKI MARUTI/STW | | | 24/04/2001 |
| 5. | SU 33468 | MITSUBISH L 200 | 4D56JB6365 | JMYJNK340WP003344 | 13/02/1998 |
| 6. | SU 35602 | MITSUBISH | 4D56BG9274 | MMBONK7403D042066 | 23/04/2003 |
| 7. | SU 33448 | MITSUBISH | 4D56JB4664 | JMYJNK340WP003119 | 13/02/1998 |
| 8. | SU 26442 | T0Y0TA L/CRUISER | | | 22/09/1989 |
| 9. | SU 33565 | MARCEDEZ-BENZ | 3.56909E+12 | WDB6751472K274936 | 14/05/1996 |
| 10. | SU 29149 | TATA TRUCK | 697P21995114 | 3.68021E+11 | 17/12/1991 |
| 11. | SU 33661 | MITSUBISH TRUCK | 4D32G08698 | FG635EC00325 | 11/09/1998 |
| 12. | SU 33638 | MITSUBISH TRUCK | | | 11/09/1998 |
| 13. | SU 33514 | TATA TRUCK | 495D21R0SQ744315 | MAT379040V8R12385 | 4/03/1998 |

217024302

Inaendelea Uk. 8

# TANGAZO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 14. | SU 32837 | TATA TRUCK | 497D21LUQ802799 | MAT379040T8R02073 | 17/06/1996 |
| 15. | SU 27556 | TRAILER | | | 9/06/1999 |
| 16. | SU 36691 | QINGQI | CG125E-2210654 | CG125-1623936 | 3/08/2006 |
| 17. | SU 36654 | QINGQI | 157FM0621000020 | LAFLYZ4066B930013 | 2/08/2006 |
| 18. | SU 34297 | SUZUKI TF 125 | TF125/138204 | TF125/137881 | 24/04/2001 |
| 19. | SU 34296 | SUZUKI TF 125 | TF125/137979 | TF125/137563 | 22/06/2000 |
| 20. | SU 35703 | QINGQI | 157FMI0221001030 | LAELYZ40338930109 | 29/07/2003 |
| 21. | SU 36690 | QINGQI | 157FMI0421001343 | LAELYZ4026B930025 | 3/08/2006 |
| 22. | SU 33731 | HONDA XL 125 | LI265E5561040 | LI255/5713346 | 4/02/1999 |
| 23. | SU 32189 | SUZUKI YAMAHA | 3HA/033952 | 3HA/033952 | 2/02/1995 |
| 24. | SU 32924 | YAMAHA G 100 | 3HA/033467 | 3HA/033437 | 19/08/1996 |
| 25. | SU 33357 | YAMAHA DT 125 | 8TT/055186 | 3TT/034758 | 24/09/1997 |
| 26. | SU 33733 | HONDA XL 125 | LI255E5561038 | LI255/57103345 | 4/02/1999 |
| 27. | SU 28300 | HONDA XL 125 | LI255E5532414 | LI255/5420578 | 11/05/1998 |
| 28. | SU 30159 | HONDA 110 | JDOTE2000398 | JDO1/5100416 | 24/08/1992 |
| 29. | SU 33547 | HONDA XL 125 | LI85SE/5436229 | LI85S/6000321 | 11/05/1998 |
| 30. | SU 24224 | HONDA CG 125 | CG125E1894642 | CG1251400359 | 11/05/1998 |

**KITUO NA. 11– SINGIDA – 3/10/2022**
**31. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA SINGIDA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 31576 | L/ROVER | 11L-38285A | SAUDHMF7CA 934764 | 1994 |
| 2. | SU 33488 | MITSUBISH PICK UP | 4D5WB4927 | JMYJMK340WP003142 | 1998 |
| 3. | SU 34859 | MITSUBISH PICK UP | 4D56AZ7099 | MMBONK740ZD020687 | 2002 |
| 4. | SU 35701 | QINGQI | 157FM10221000930 | LAELYZ4013B930111 | 2003 |
| 5. | SU 35705 | QINGQI | 157FM10221000881 | LAELYZ4033B930112 | 2003 |
| 6. | SU 36692 | QINGQI | 157FM106221000013 | LAELYZ4066B930044 | 2006 |
| 7. | SU 36693 | QINGQI | 157FM10221001017 | LAELYZ4056B930035 | 2006 |
| 8. | SU 35706 | QINGQI | 157FM10221000863 | LAELYZ4063B930105 | 2003 |

**KITUO NA. 12 – TABORA – 5/10/2022**
**9. VIFAA CHAKAVU MCHANGANYIKO MBALIMBALI NA MAGARI YA TABORA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 26968 | SUZUKI SAMURAI | 4D56BL5632 | MMBJNK7404D007920 | 1998 |
| 2. | SU33572 | BENZ CRANE | 3.5 6909E+13 | WDB6751472K2742828 | 1998 |
| 3. | SU 33660 | MITSUBISH TRUCK | 4D32908926 | E9635EC00326 | 1998 |
| 4. | SU 23949 | BENZ TRUCK | 35290620554379 | WDB353102-25-325898 | 1987 |
| 5. | SU 34425 | LAND ROVER TDI 300 | 16L-21405A | SALLD4MF7MD-964891 | 1995 |
| 6. | SU 33413 | LAND ROVER DEFENDER | 11L26700A | SMDHMFIJA921865 | 1993 |
| 7. | SU 33508 | TATA TRUCK | 497D21RLTQ824405 | MAT379040T8R40466 | 1997 |
| 8. | SU 35801 | MITSUBISH L 200 | MISSING | MMBJNK7404D007505 | 2003 |
| 9. | SU 33483 | MITSUBISH L 200 | 4D56JB4495 | DMIJNK340WP0J3112 | 1997 |
| 10. | SU 34359 | SUZUKI TF 125 S | 139072 | TF 125 138676 | 2001 |
| 11. | SU 32930 | YAMAHA | 3HA033434 | 3HA033434 | 1995 |
| 12. | SU 32929 | YAMAHA | 3HA033418 | 3HA033418 | 1995 |
| 13. | SU 36702 | QINGQI | 157FMI0621000028 | LAELYZ4096B930037 | 2006 |
| 14. | SU 32928 | YAMAHA | 3H033415 | 3H033415 | 1995 |
| 15. | SU 36703 | QINGQI | 157FMI0621000024 | LAELYZ40 86B930031 | 2006 |
| 16. | SU 34358 | SUZUKI TF 125 S | TF 125 139174 | TF125 138879 | 2001 |
| 17. | SU 35708 | QINGQI | 157FMI 0221000983 | LAELYZ40 23B930103 | 2002 |
| 18. | SU 35710 | QINGQI | MISSING | LAELYZ40 23B930070 | 2002 |
| 19. | SU 32166 | YAMAHA | MISSING | 3HA 033947 | 1993 |

**KITUO NA. 13 – KATAVI – 7/10/2022**
**20. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KATAVI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 31027 | LAND ROVER DEFENDER | 11L16518 | SLLDHMF75A909220 | 1992 |
| 2. | SU 36677 | QINGQI | 157FMI-06221001005 | LAELYZ4016D930050 | 2002 |
| 3. | SU 32926 | YAMAHA | 3HA033419 | 3HA033419 | 1995 |
| 4. | SU 33736 | HONDA XL 125S | L125SE5561067 | L125S 5713322 | 1998 |

**KITUO NA. 14 – KIGOMA – 9/10/2022**
**5. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KIGOMA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 35817 | MITSUBISH L200 | 4D56BL5632 | JMYGWK340WP003368 | 2003 |
| 2. | 2SU 33485 | MITSUBISH L200 | 4D56JB4872 | MG71-IN-0208685 | 1997 |
| 3. | SU 36700 | QINGQUI | 157FMI-0621000006 | LAELYZ40X6B930 | 2006 |
| 4. | SU 36701 | QINGQUI | 157FMI-0221000922 | LAELYZ4056D930 | 2006 |
| 5. | SU 34362 | SUZUKI TF 125W | 139248 | 138917 | 2001 |

**KITUO NA. 15 – SHINYANGA – 11/10/2022**
**6. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA SHINYANGA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 34863 | MITSUBISH P/UP | 4D56BA2609 | MMBJNK7402DOZ5024 | 2002 |
| 2. | SU33484 | MITSUBISH P/UP | 4D56J84737 | JMYJNK340WP003129 | 1998 |
| 3. | SU 35799 | MITSUBISH 4LD | K 74TJENSR | MMBJNK7404D007346 | 2003 |
| 4. | SU 36694 | QINGQI | 157FMI 022100874 | LAELYZY4073B9130078 | 2002 |
| 5. | SU32165 | YAMAHA | 3HA 033948 | 3HA 033948 | 1993 |
| 6. | SU 34355 | | TFR 513986 | TF125 138867 | 2001 |
| 7. | SU 34354 SUZUKI | | TF 125 139245 | TF 125 138915 | 2001 |
| 8. | SU 3711 QINGQI | | 157 FMI 0321000089 | LAELYZ40168930047 | 2003 |

**KITUO NA. 16 – MWANZA – 13/10/2022**
**9. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI**

**KITUO NA. 17 – KAGERA – 15/10/2022**
**10. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KAGERA**

| | | | KAGERA | |
|---|---|---|---|---|
| S/N | REG.NO. | MAKE | MODEL | YEAR |
| 1. | SU 35907 | ISUZU | PICK UP | 2003 |
| 2. | SU 35901 | ISUZU | TRUCK | 2000 |
| 3. | SU 29482 | TOYOTA | PICK - UP | 1991 |
| 4. | SU 35825 | MITSUBISHI | PICK - UP | 2003 |
| 5. | SU 32979 | TOYOTA | PICK - UP | 1996 |

**KITUO NA. 18 – GEITA 17/10/2022**
**6. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA PIKIPIKI YA GEITA**

| | | | GEITA | |
|---|---|---|---|---|
| S/N | RG. NO. | MAKE | CHASIS NO. | YEAR |
| 1. | SU 34334 | SUZUKI | TF 125W | 2001 |

**KITUO NA. 19 – MARA– 19/10/2022**
**2. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MARA**

| S/N | REG. NO. | MAKE | CHASIS NO. | YEAR |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 36094 | YAMAHA | 125 R | 2004 |
| 2. | SU 32299 | YAMAHA | DT125 | 1995 |
| 3. | SU 34365 | SUZUKI | TF 125W | 2001 |
| 4. | SU 35724 | QINGQI | QINGQI | 2003 |
| 5. | SU 35725 | QINGQI | QINGQI | 2003 |
| 6. | SU 32295 | YAMAHA | DT125 | 1995 |
| 7. | SU 32296 | YAMAHA | DT125 | 1995 |
| 8. | SU 32298 | YAMAHA | DT125 | 1995 |
| 9. | SU 32297 | YAMAHA | DT125 | 1995 |
| 10. | SU 35726 | QINGQI | QINGQI | 2003 |
| 11. | SU 36697 | QINGQI | QM125GY-2 | 2006 |
| 12. | SU 33747 | HONDA 125 | | 1996 |
| 13. | SU 28700 | HONDA 125 | | 1991 |

Inaendelea Uk. 9

# TANGAZO

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 14. | SU 33664 | MITSUBISH | TRUCK | 1998 |
| 15. | SU 33472 | MITSUBISH | PICK UP | 1997 |
| 16. | SU 36067 | TOYOTA | PICK UP | 2004 |
| 17. | SU 33327 | FIAT | TRUCK | 1997 |
| 18. | SU 30729 | L/ROVER | S/WAGON | 1993 |
| 19. | SU 33512 | TATA | TRUCK | 2003 |

**KITUO NA. 20 – SIMIYU– 21/10/2022**
**20. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA SIMIYU**

SIMIYU

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 123 | SU 34356 | SUZUKI | TF125 | 2001 |
| 124 | SU 35744 | QUINQUI | QM125GY-2 | 30/06/2003 |
| 125 | SU 35745 | | | 30/06/2003 |
| 126 | SU 36695 | | | 2003 |
| 127 | NO. REG. NO | QUINQUI | | |

**KITUO NA. 21 – MANYARA – 23/10/2022**
**21. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MANYARA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 32692 | TOYOTA HILUX | 3L3927311 | LN1060122015 | 26/03/1996 |
| 2 | SU 35621 | T/L/CRUSER | 1HZ0117705 | HZJ750020033 | 29/04/2003 |
| 3 | SU 34003 | MITSUBISH L 200 | 4D56J56243 | JMY0NK340WP002658 | 29/11/1999 |
| 4 | SU 33737 | HONDA XL 125 | L125FS-5561020 | L125C-5713324 | 4/02/1999 |
| 5 | SU 35704 | QINGQ | 157FM10221001039 | LAELYZ40X3B930107 | 29/07/2003 |
| 6 | SU 35714 | QINGQ | 157FM10221000883 | LAELYZ4043B930071 | 30/07/2003 |
| 7 | SU 35717 | QINGQ | 157FM10221001045 | LAELYZ4063B930086 | 30/07/2003 |
| 8 | SU 36688 | QINGQ | 157FM10621000026 | LAELYZ40X6B930015 | 3/08/2016 |

**KITUO NA. 22 – ARUSHA – 25/10/2022**
**22. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA ARUSHA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 40767 | HLUX-D/CABIN | 2KDA662633 | AHTFR22G906098239 | 19/08/2015 |
| 2. | SU 33447 | MITSUBISH PICK-UP | 4D56JB3749 | JMUNK340WP003117 | |
| 3. | SU 33467 | MITSUBISH PICK-UP | 4D56JB6314 | JMYJNK340WP003360 | 13/02/1998 |
| 4. | SU 36286 | MITSUBISH CANTER | 4D32K30333 | FE645EA46258 | 12/07/2005 |
| 5. | SU 435713 | QINGQI | 157FM10221000912 | LAELYZ4013B930075 | 30/07/2003 |
| 6. | SU 32066 | YAMAHA | 3HA033244 | 3HA033244 | 24/11/1994 |
| 7. | SU 35715 | QINGQI | 157FM10221000885 | LAELYZ4063B930072 | 30/07/2003 |
| 8. | SU 36686 | QINGQI | 157FM10621000009 | LAELYZ4096B930023 | 3/08/2006 |
| 9. | SU 34297 | SUZUKI | 137817 | 137660 | |
| 10. | SU 35716 | QINGQI | 157FM10221001010 | LAELYZ4823B930098 | 30/07/2003 |

**KITUO NA. 23– KILIMANJARO – 27/10/2022**
**11. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KILIMANJARO**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 33466 | MITSUBISH P/UP | 4D56JB6491 | JMYGWK340WP00 3368 | 13/02/1998 |
| 2. | 34309 | SUZUKI MARUTI | 913BBN-111345 | MG71-IN-0208685 | 30/06/2001 |
| 3. | 27640 | TATA TRUCK | 097SP21926679 | 368020927304 | 8/09/1990 |
| 4. | 27950 | TATA TRUCK | 697-SP21-9-43121 | 368-020-9-33248 | 30/06/1996 |
| 5. | 24526 | HONDA | CG125E-1894629 | CG1251400330 | 12/02/2022 |

**KITUO NA. 24 – NYUMBA YA MUNGU – 29/10/2022**
**6. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI**

**KITUO NA. 25 – PANGANI – 31/10/2022**
**7. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA PANGANI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 34118 | T/HILUX D/CABIN | 2L1512335 | LN410004333 | 1993 |
| 2. | SU 35617 | T/HILUX D/CABIN | | LN1060014671 | 1992 |
| 3. | SU 33711 | T/L/CRUSER | 2H1204043 | HJ6049275 | 14-Jun-05 |
| 4. | SU 36671 | QINGQI | 157FMI062000005 | LAELYZ4086B930045 | 1991 |
| 5. | SU 35618 | HONDA 110 | JD01E2404227 | JD015301362 | 2006 |
| 6. | SU 36670 | QINGQI | 157FMI0621000001 | LAELYZ4076B930022 | 2006 |

**KITUO NA. 26 – TANGA – 2/11/2022**
**7. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA TANGA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | YEAR OF PURCHASE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | SU 35803 | MITSUBISH PICK-UP | 4D56BL4105 | MMBJNK7404D007503 | 15.09.2003 |
| 2. | SU 40799 | T/HILUX D/CABIN | 2KDA643475 | AHTFR22G206096722 | 18.08.2014 |
| 3. | SU 36071 | MITSUBISH D/CABIN | 4D56BN1869 | MMBJNK7404002604 | 16.07.2004 |
| 4. | SU 34306 | SUZUKI MARUTI | G13BBN111366 | MJ711N0208686 | 14.02.2008 |
| 5. | SU 34285 | SUZUKI | 137841 | X137663 | |
| 6. | SU 35694 | QINGQI | 157FM10221000955 | LAELYZ4043B930099 | 29.07.2003 |
| 7. | SU 34289 | SUZUKI | | TF125-137676 | 20.04.2001 |
| 8. | SU 33437 | FOCAL LIFT | FD1002-7693376BD1PD-03AD/JH | 00 559 | |

**KITUO NA. 27: NJOMBE Tarehe 4/11/2022**
**9. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA NJOMBE**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 33475 | MISTUBISHI PICK UP L200 | | V5M214625 |
| 2 | SU 34862 | MISTUBISHI PICK UP L200 | | V5M214875 |
| 3 | SU 35732 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | | LAELYZ40938930123 |
| 4 | SU 34358 | SUZUKI MOTOR CYCLE | 139174 | TF125138916 |

Inaendelea Uk. 10

# TANGAZO

**KITUO NA. 28: KIHANSI Tarehe 6/11/2022**
**10. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA KIHANSI**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 35090 | TOYOTA LAND CRUSER | 1HZ0037771 | HZGA75-0025334 |
| 2 | SU 33264 | TOYOTA GX | 1HZ02011890 | HZGA80-0030942 |
| 3 | SU 33651 | DIANER PAC | 4D32G09724 | 4801734 |
| 4 | SU 35623 | MOTAR CYCLE- YAMAHA | 3TT025915 | 3TT-025915 |
| 5 | SU 35614 | MOTAR CYCLE- YAMAHA | 3TT082064 | 3TT-039064 |
| 6 | SU 35092 | MOTAR CYCLE- YAMAHA | 3TT039003 | 3TT-039003 |
| 7 | SU 35095 | MOTOR CYCLE-HONDA 110 | JD01E2420927 | D01-5306496 |
| 8 | SU 36669 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI0221001034 | LAELYZ4046*B390026* |

**KITUO NA. 29: IRINGA Tarehe 8/11/2022**
**11. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA IRINGA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 33271 | TATA TRUCK | 497D21KTQ815380 | MAT379040T5R70282 |
| 2 | SU 33642 | MITSUBISH CENTER | 4D32G10845 | FG635EC00348 |
| 3 | SU 35822 | MISTUBISHI PICK UP | 4D56BL5637 | MMBJNK7404D008026 |
| 4 | SU 32912 | TATA TRUCK | 497D2142836 | MAT37904014584 |

**KITUO NA. 30: MBEYA Tarehe 10/11/2022**
**12. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA MBEYA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 33665 | MITSUBISHI | 4D32G08811 | FG635EC00324 | 11.09.1988 |
| 2 | SU 33337 | TATA TRUCK | 497D21MTQ834275 | MAT379040T5R70505 | 22.08.1997 |
| 3 | SU 33270 | TATA TRUCK | 497D21KTQ815210 | MAT379040T5R70281 | 27.06.1997 |
| 4 | SU 33474 | MITSUBISHI PICKUP | 4D56JB5263 | JMYJNK340WP003201 | 13.02.1998 |
| 5 | SU 34322 | SUZUKI -MARUTI | G13BBN111291 | MG711N0208667 | 30.04.2001 |
| 6 | SU 33758 | BENZI | MJ03033SA103392C | ABD39737226003361 | 1998 |
| 7 | SU 31072 | TATA TRUCK | 692D22411547 | 3580397794 | 24.05.1993 |
| 8 | SU 35730 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI0221000971 | LAELYZ40X3B930110 | 30.07.2003 |
| 9 | SU 35727 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI10221000867 | LAELY204138930125 | 30.07.2003 |
| 10 | SU 35344 | MOTOR CYCLE SUZUKI | T125-138060 | TF125-137838 | 08.05.2001 |
| 11 | SU 35728 | MOTOR CYCLE QUINGQI | 157FMI0221001046 | LAELYZ4033B930126 | 30.07.2003 |
| 12 | SU 33841 | MOTOR CYCLE HONDA | L125SE5562384 | L125S5714437 | 08.04.1999 |
| 13 | SU 36674 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FM/1032100334 | QM125GY2 | 02.08.2006 |
| 14 | SU 33014 | MOTOR CYCLE HONDA | | | 08.10.1996 |
| 15 | SU 33752 | MOTOR CYCLE HONDA | L125S5560673 | L125S5713136 | 08.04.1999 |
| 16 | SU 36675 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI10621000027 | LAELYZ4096B930006 | 02.08.2006 |
| 17 | SU 33013 | MOTOR CYCLE HONDA | L125SE5547689 | L125S5707492 | 08.10.1996 |
| 18 | SU 33751 | MOTOR CYCLE HONDA | L125SE5560661 | L125S5713084 | 10.02.1999 |
| 19 | SU 30623 | LEYLAND | L08865 | 606747 | 17.12.1992 |
| 20 | SU 35819 | MISTUBISHI | 4D56BL4119 | MMBJNK7404D007957 | 17.09.2003 |
| 21 | SU 35729 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI0221000947 | LAELYZ40438930 | |

**KITUO NA. 31: RUKWA Tarehe 12/11/2022**
**13. VIFAA CHAKAVU MBALIMBALI NA MAGARI YA RUKWA**

| S/N | REG. NUMBER | MAKE/MODEL | ENGINE NUMBER | CHASIS NUMBER |
|---|---|---|---|---|
| 1 | SU 36676 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 15FM1*06212000016* | LAELYZ4056B23930021 |
| 2 | SU 35749 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 15FM*10221001002* | LAELYZ40X35B930091 |
| 3 | SU 35886 | MOTOR CYCLE-QUINGQI | 157FMI10221000984 | LAELYZ4063B930136 |

## MASHARTI YA MNADA

1. Chombo/Kifaa kitauzwa kama kilivyo na mahali kilipo;

2. Mnunuzi atalazimika kulipa papohapo amana (deposit) isiyopungua asilimia ishirini na tano (25%) ya thamani ya Chombo/Kifaa alichonunua, na kukamilisha malipo yote katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti hili atakosa haki zote za ununuzi wa Chombo/kifaa husika na amana iliyolipwa haitarudishwa;

3. Mtu yeyote atakaye tamka bei ya juu kisha akashindwa kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei aliyotamka, atachukuliwa kuwa ni mwenye kutaka kuvuruga mnada na hivyo hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake kwa mujibu wa sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

4. Mnunuzi atatakiwa kuondoa/kuchukua chombo alichonunua katika muda wa siku saba (7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo;

5. Vyuma Chakavu vitauzwa kwa Wanunuzi wenye viwanda vya kuchakata chuma tu. Wanunuzi wa vyuma chakavu watatakiwa kuleta leseni za kuchakata chuma na leseni hizo zitakaguliwa kabla ya zoezi la mnada kuanza. Vile vile nakala ya leseni hiyo itabaki kwa Muuzaji kwa ajili ya kumbukumbu;

6. Gharama za kubadilisha umiliki ni jukumu la mnunuzi na atatakiwa kukamilisha taratibu za kumilikishwa chombo/kifaa/chuma chakavu alichonunua kwa mujibu wa Sheria ndani ya siku ishirini na moja (21);

7. Ruhusa ya kuangalia vyombo itatolewa siku (5) kabla ya tarehe ya mnada husika;

8. Mnada utaanza saa nne (04:00) kamili asubuhi katika kila kituo kwa mtiririko uliooneshwa; Kwa vituo vyenye vituo vidogo yani A na B mnada utaanza kituo A kufuatia B.

9. Wananchi wote mnakaribishwa kushiriki katika mnada huu wa hadhara.

**IMETOLEWA NA**
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**SHIRIKA LA UGAVI WA UMEME TANZANIA (TANESCO)**

ama
AFYA NA MAZINGIRA
ALHAMISI SEPTEMBA 1, 2022



Ukurasa 12

## Wataalamu NEMC wasimulia vimiminika taka vinavyochochea uchafuzi mazingira

## HISTORIA KUU KUMTUA MAMA NDOO

## Waziri Aweso 'mguu kwa mguu' na Sh.Trilioni moja kuifikishia maji miji 28



Ukurasa 13

# Njia tano za kutunza ngozi yako kiasilia, yenye afya, bila gharama

Na Dk. Mussa Zaganza

NGOZI ni kinga muhimu katika afya ya mwanadamu, ikiwamo kuwa kinga ya mwili. Lakini ina hitaji muhimu la kutunzwa kwa ufasaha na asilia kwa namna zote. Kitaalamu, suala la tiba ya ngozi kwa umuhimu wa kwanza, kila mtu anapaswa kuondoa mawazo, ni namna gani anapaswa kuitunza.

Muhimu cha kwanza, ni kwamba, watu wanatakiwa kuondoa fikra kwamba, ili kuwa na ngozi yenye afya ni lazima awe na vipodozi vingi, kinyume chake anapokuwa na vipodozi vingi, hasa vya wazalishaji tofauti, baadhi yake haviendani pamoja na kitaalamu inaitwa 'incompatible', hata kuzidi kuharibu ngozi zaidi.

Hivyo, kuepuka madhila hayo na mengine yanayofanana nayo, kuna mambo makuu matano ya kuzingatia, ikiwamo pale inapowezekana kutumia mafuta ya aina moja tu.

Mazoezi:Ngozi ya binadamu ni kiungo kinachopumua kupitia vinyweleo, ikihitaji jasho lipite. Kama shughuli za mtu ni za kukaa muda mrefu, anapaswa kutembea kwa namna tofauti, iwe kutembea au mazoezi. Ni hali inayofanya ngozi inakaza na mikunjo kuondoka.

Kula matunda na mboga kwa wingi; vitamini zote zinazohitajika kwa afya ya ngozi, zipo kwenye matunda ikiwemo vitamini E. Kwa hiyo, kwani hata mafuta ya ngozi au losheni zipo zinazoongezewa vitamini E kukabili uhaba wake kwenye ngozi.



Sehemu za ngozi zilizopata madhara. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Pia, kuna tahadhari ya vitamini E kwa wanaokunywa vidonge, ili wapate matokeo ya haraka ya ngozi na nywele ndefu, bila kujua athari za baadaye za kunywa vidonge hivyo. Ni rahisi mtu anayeishi shamba kuwa na ngozi nyororo, kushinda wa mjini, kwa sababu wa mjini, muda mrefu hula vitu vya sukari kama 'lamba lamba'. Muhimu ni kuwa na ratiba ya kula tunda kila siku.

Kunywa maji ya kutosha; mtu kama hanywi maji ya kutosha, ngozi yake kujenga makunyanzi na michirizi. Kunywa maji ya kutosha, kunaifanya ngozi ing'are kwa rangi yake ya asili.

Wataalam wameweka muongozo wa kiasi cha maji mwili unahitaji kwa masaa 24. Muhimu mtu asinywe kiasi kikubwa kwa mara moja, bali glasi kwa awamu, hali inayorahisisha kuondoa sumu nje ya mwili kupitia kibofu (mkojo).

Mtu anaelezwa pale anaposhindwa ratiba ya kunywa maji, basi aweke glasi nane kwenye chupa moja kila asubuhi awe anakunywa taratibu na amalize, inapotimu asubuhi inayofuata, awe amemaliza maji ya mwanzo.

Kupumzika na kupata usingizi wa kutosha; inatajwa hali ya kukosa usingizi kila mara kunashusha kinga ya mwili, hivyo kunafanya ngozi izeeke mapema.

Mchana mtu anapofanya kazi, damu inayobeba lishe zote kama vitamini E na protini inatumika kuhudumia maeneo muhimu ya mwili kama vile ubongo, ini, mapafu, moyo wenyewe, macho, misuli ya miguu na mikono.

Hapo mtu anapolala, damu yake inakosa kazi nyingi na kwenda maeneo yaliyosahaulika mchana, ikiwemo ngozi. Kadri mtu anavyopumzika vya kutosha, anaipa ngozi fursa ya kusambaziwa lishe na damu, hivyo lazima itang'ara.

Kuna jambo la kujiuliza kati jamii zetu, je mnawajua mabinti wanaowekwa ndani kabla hawajaolewa, wakiitwa Wali? Pa kujiuliza, wanapotoka huko ngozi zao zinakuwaje?

Hapo, kitaalamu ni kwamba mtu kama ana ugonjwa wa kukosa usingizi, anapaswa kujitibu kwanza, vinginevyo, anaweza kuhangaika kusaka mbadala wa kujitibu ngozi kwa kununua vinakishi (cosmetics) kwa wingi, bila kupata matokeo chanya.

Kutumia mafuta na vipodozi asilia; kuna vipodozi mtu anaweza kuviandaa hata akiwa nyumbani, mfano kukamua mafuta ya nazi. Ngozi inapokuwa tayari imeshapoteza unyororo wake, kunahitajika kurudishwa kwa njia asilia, ili kuipa kinga na yenyewe kurudi kuwa nyororo

**** Mwandishi ni mtaalamu wa afya ya ngozi na nywele kutoka taasisi Natural Skin Solution. Kwa ushauri wasiliana kwa simu: 0713 039875. Pia, kupata jibu la kitaalamu kuna mtandao wa 'online clinic' kuwasaidia Watanzania afya ya ngozi na nywele. Wasiliana kwa kupiga simu au 'whatsapp' ya namba iliyopo, kupata ushauri bure.***

MAZINGIRA

# Wataalamu NEMC wasimulia vimiminika taka vinavyochochea uchafuzi mazingira

## •Vimetapakaa kona zote, shida ni kuvitambua

**Na Joseph Mwendapole**

MUUNDO wa maisha na hasa kwa binadamu, yana pilika nyingi. Daima katika harakati zao kutafuta maslahi na hasa ya kiuchumi, huwa anasahau umuhimu wa kuweka mazingira kwenye hali sahihi kwa manufaa yake na vizazi vijavyo, viikute katika hali nzuri

Pia, inagundulika shughuli alizo nazo zimemfanya mwanadamu kusahau jukumu kubwa alilo nalo la kuthamini, kuhifadhi na kuyatunza mazingira yake.

Hapo kuna marejeo kwamba, zipo shughuli nyingi zinazofanywa zikiwamo za migodini, viwandani, hospitalini, mashambani, majumbani na zinginezo ndiyo chanzo cha taka zinazochafua na kuathiri mazingira na mwishowe kuzua mlipuko wa magonjwa.

Kuna maradhi kama vile kipindupindu, kichocho, dengue na athari zake kwenye mazingira zinatajwa kuwa ni kuharibika ikolojia za wanyama na mimea, pamoja na kuondoshwa hewa safi kutokana na harufu mbaya.

MAOFISA NEMC

Ofisa Mazingira Daraja la Kwanza wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Obasanjo Nniwako, anataja Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, anataja taka zenye madhara, ni kitu chochote kigumu, majimaji au ya gesi.

Hapo anaeleza kwamba sababu ni athari zake, kiwango chake cha sumu na ulipukaji wake unadhuru afya, maisha ya binadamu au hata mazingira jirani.



Sehemu ya viminika ambavyo vinachafua mazingira. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Anafafanua tafsiri ya msingi ya taka inagusa taka zozote zilizoko katika hali ya gesi au majimaji, zitokanazo na shughuli kama za viwandani, migodini, biashara, kilimo na majumbani, ambazo zinaweza kuwa na madhara kwa mazingira na afya ya binadamu.

Hiyo ni pale ama zisipomwagwa au kuhifadhiwa kwa utaratibu maalum salama, ili zisisambae na kufika mbali, hata kuwa na athari za namna tofauti.

Anasema taka miminika zitokanazo na shughuli za majumbani na biashara, zinaweza kuwa za asili ya majitaka, uoshaji vyombo majumbani na kuambatana na mabaki ya vyakula, kufua nguo kwa sabuni inayotengeneza povu jingi.

Pia, Obasanjo anataja mifano yake ni kama kemikali inayotumika kuosha nywele saluni, maji ya kuosha matunda au mboga sokoni, maji na kuunganishwa kwa mfumo wa maji kiholela.

Mtaalamu huyo wa NEMC anasema, kundi hilo la vimiminika taka huweza kusababisha kichocheo kikubwa cha mazalia ya wadudu, pia vimelea vya magonjwa mbalimbali kama vile kipindupindu, dengue, malaria na homa ya tumbo.



Anaeleza, kuna wakati inachangia kwenye mlipuko wa magonjwa yasiyo ya kuambukiza, kutokana na eneo hilo kuathirika na taka miminika, ikabadilisha hali ya hewa kwa harufu, joto na mifumo ya ikolojia.

Obasanjo ana ufafanuzi kuwa vimiminika taka vitokanavyo na shughuli za viwandani, hospitali na kilimo, huzalisha majitaka yatokanayo na mfumo wa utengenezaji bidhaa, mafuta machafu ya kulainishia mitambo, moshi na kemikali zilizochanganyika na maji.

Anasema, shughuli za matibabu hospitalini zinazalisha vimiminika taka kama vile majitaka yatokanayo na kusafishia vidonda vya wagonjwa, vifaa tiba, majitaka vyooni, mabaki ya dawa za maji na gesi, kutoka mitambo ya kutibu wagonjwa.

Mwanamazingira Obasanajo, anasema shughuli za kilimo zinazalisha vimiminika taka vitokanavyo na matumizi ya viatilifu, dawa za kupandia, kukuza na kuua magugu hususani yanapochanganyikana na maji au na hewa.

Kwa mujibu wa ofisa huyo wa NEMC, vimiminika taka kutoka kundi hilo vinaweza kuleta madhara mbalimbali kwa mazingira na wanyama, yakiwemo magojwa ya miwasho, saratani na kuongezeka viumbe vamizi.

Mengine anayoyataja ni kubadilika ikolojia ya viumbe, tabaka la hewa safi na kusababishwa mabadiliko ya hali ya hewa, hususani joto na vifo vya viumbe hivyo.

Kwenye vimiminika taka vitokanavyo na shughuli za migodi, anaeleza kwamba ni kundi linalozalisha vimiminika taka kama vile, tope sumu, maji asidi, mafuta machafu, madini tembo, gesi sumu na maji taka toka vyooni.

Anataja madhara yanayoweza kusababishwa na kundi hilo la vimiminika taka ni pamoja na kuwashwa, kubabuka ngozi, saratani, hata vifo na mabadiliko ya vinasaba kwa viumbe hai, akiwemo kibadamu, huku kukiwapo uongezeko la viumbe vamizi vinavyobadili ikolojia ya viumbe na mazingira kwa ujumla.

AINA YA UCHAFUZI

Ofisa Mazingira mwingine kutoka NEMC, Ramadhani Shausi, anasema uchafuzi kwa taka miminika, uhalisia wake hautofautiani sana na uchafuzi wa maji taka kwa maana na mtazamo wa uharibifu wa mazingira ambayo kwa hakika yake ni mchanganyiko wa kinyesi, mikojo, uchafu na majitaka yatokanayo na uzalishaji na shughuli za majumbani.

Anabainisha kuwa shughuli za asasi au biashara mazingira haya huharibiwa sana na matokeo ya shughuli za binadamu zinazozalisha taka vimiminika hizo zinazoambatana wakati mwingine na kemikali isiyo rafiki kwa ardhi na kuharibu ikolojia nzima ya mazingira, hewa safi na afya.

"Ni ukweli usiopingika kabisa kwamba mazingira safi na salama ni afya, hupendeza machoni, huvutia watalii, huimarisha mimea, hunufaisha viumbe hai na hata ndege wa angani..." anasema na kuongeza:

"Kwa maana hiyo, taka vimiminika hizi zinatakiwa kuhifadhiwa kwa utaratibu ulio rafiki utakaowezesha kuhifadhi na kutunza mazingira kwa maslahi mapana ya Nchi na Taifa kwa ujumla."

Anasema kuna umuhimu wa kuepuka kumwaga taka vimiminika hovyo ili tuyatunze na kuyahifadhi mazingira yetu na tuyatunze mazingira ili yatutunze.

MAZINGIRA

### HISTORIA KUU KUMTUA MAMA NDOO KICHWANI

# Waziri Aweso ‘mguu kwa mguu’na Sh. Trilioni moja kuifikishia maji miji 28

## •Timu wizara yajipanga ‘wasizingue’ mradi ulioshuhudiwa saini yake Ikulu

**Na Renatha Msungu**

HADI sasa nchini kunatajwa kuwapo huduma ya maji kwenye miji 28 nchini, yenye jumla ya thamani Dola za Marekani milion 500, inayotekelezwa na serikali ili kukabili tatizo la maji,mijini na vijijini. Matarajio yanajumuisha, kupunguza magonjwa ya mlipuko kitaifa.

Ufafanuzi wa Wizara ya Maji, ni kwamba, Watanzania takribani milioni sita watanufaika, kwa kuimarishiwa

huduma ya majisafi na salama, ikiwa ni mradi wa kihistoria na alama kubwa Sekta ya Maji kitaifa.

Miji inayoingia katika orodha hiyo na mikoa yao katika mabano ni: Handeni, Muheza na Pangani (Tanga); Kilwa Masoko (Lindi); Newala na Nanyumbu (Mtwara); Ifakara (Morogoro), Chunya (Mbeya); Geita na Chato (Geita); na Songea (Ruvuma).

Miji mingine ni: Njombe, Rujewa, Makambako, na Wanging’ombe (mkoa Njombe); Mafinga (Iringa), Mpanda (Katavi); Sikonge, Urambo na Kaliua (Tabora), Singida, Manyoni (Singida); Chemba na Chamwino (Dodoma), Kasulu (Kigoma); Kayanga (Kagera),pia Rorya na Tarime mkoani Mara.

Ni hatua inayoendana na dhana ‘kumtua mama ndoo kichwani’ uwekezaji wa mradi tajwa ukielezwa ni wa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Exim ya nchini India, ambayo ni sawa na shilingi trilioni moja za nchini.

Serikali ya India ambayo imefanikisha mkopo huo, imekuwa mdau mkubwa wa kusukuma maendeleo ya umma katika sekta ya maji, ikitumika kuijengea uwezo wataalamu nchini, miradi ya namna hiyo kuwa endelevu kuhudumia umma.

Ushirikiano baina ya India na Tanzania katika maendeleo, inatajwa kuwa kielelezo dhahiri katika sekta ya Maji, pia ni mradi mkubwa wa maji kati ya Tabora- Igunga - Nzega

uliokamilika wenye thamani ya shilingi bilioni 600 na sasa unafaidisha zaidi ya watu milioni 1.2.

**WANAOONGOZA WIZARA**

Waziri wa Maji Jumaa Aweso, anasema Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Exim ya India, Gaurav Bhandari katika safari ya kikazi nchini, kwenye moja ya vikao vyake na watendaji wa sekta ya maji, aliainisha uhusiano kati ya India na Tanzania ni mkubwa, pia ni wa siku nyingi, akifafanua mradi wa maji wa miji 28, unatekelezwa na kampuni anayoitaja itakuwa bora.

Anafafanua, kandarasi ya mradi imetolewa kwa kampuni tofauti, ikiwamo: JW INFR, AFCONS Infrastructures, Larsen & Toubro, Megha Engineering and Infrastructures, China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) na Jandu Plumbers, ikiwa ishara kazi itakamilika mapema na wananchi kunufaika.

Waziri Aweso anasema, Rais Samia Suluhu Hassan, ni mmoja kati ya viongozi walioshuhudia kutiwa saini mikataba na kampuni hizo, katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dodoma.

“Lengo la serikali ni kwamba ifikapo mwaka 2025, upatikanaji maji kwa maeneo ya vijijini ifikie asilimia 85 na mijini asilimia 95 na mweleko ni mzuri. Tunafanya kazi saa 24, ili wananchi wapate suluhu, hatutaki kuwa kikwazo katika jambo hili muhimu,” anaeleza Aweso.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi,

Anasema, viongozi wa sekta ya maji wamejipanga vizuri kuhakikisha mradi huo uliosubiriwa kwa muda mrefu

unafanikishwa, huku mito na maziwa itatumika kuihudumia kwa maji toshelevu.

Hapo ana msisitizo kwamba wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi, wanashirikishwa na kupokea ushauri wao kuhusu huduma ya maji kwa wananchi.

Mhandisi Anthony Sanga, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, anaufafania kuwa ni kwa wananchi wajiandae kwa kutoa ushirikiano kwa wakandarasi katika maeneo yao

**SPIKA WA BUNGE**

Spika wa Bunge Dk. Tulia Ackson, anasema wawakilishi wa wananchi kwa maana ya wabunge, wameusubiri mradi huo kwa muda mrefu tangu mwaka 2015.

Ni hoja inyoungwa mkono na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, akieleza kwamba alipoingia bungeni mwaka 2015, amekiwa akiusikia mradi huo, bila ya kuona utekelezaji wake.

Hapo anatangaza tabasamu yake, kwamba ni wakati sahihi kuu ya umma kwa muda mrefu inaenda kumalizwa, kwani hadi sasa wakandarasi wa mradi huo,

wameshaonyeshwa maeneo ya kuanza kazi katika mikoa mbalimbali nchini, hali inayoonyesha nuru ya utekelezaji mradi.



Waziri wa Maji, Jumaa Aweso.

**MPANGO KAZI**

Mpangokazi wa mwaka 2022-2023, unaonyesha Wizara ya Maji kwa upande wake umetengwa jumla ya

shilingi 657,899,338,000;, fedha za ndani shilingi 407,064,860,000 na za nje shilingi 250,834,478,000.

Vipaumbele vilivyowekwa katika kipindi tajwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi inayoendelea kutekelezwa; kuanza ujenzi wa miradi ya maji mipya ikiwemo miradi ya maji katika miji 28.

Mengine inatajwa kujumuisha ujenzi wa mabwawa ya kimkakati ya Kidunda na Farkwa, kuendelea na utunzaji wa vyanzo vya maji ikihusisha kutambua, kuweka mipaka na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali, ili vyanzo hivyo vilindwe kisheria.

Aidha, kunajumuisha kusimamia ubora wa maji na kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia vyanzo vya uhakika, ikiwamo maziwa makuu na mito mikubwa.

Kwa nchi ya Tanzania hilio linatajwa si haba, kwani kazi imefanyika sekta ya Maji. Mnamo Mei mwaka huu,Mpango wa Wizara ya Maji ulionyesha kuwa kiwango cha upatikanaji huduma ya maji kimepanda kutoka asilimia 72.3 vijijini na asilimia 86 mijini kwa mwaka 2020/21 hadi kufika asilimia 74.5 vijijini na asilimia 86.5 mjini.

Benki ya Dunia katika chapisho lake la mwaka 2022, inasema ili kuwa na uhakika wa usalama wa maji, bara la Afrika lazima liwe na maamuzi mazito kuhusu rasilimali hiyo, kwani pamoja na changamoto ya maji, bado Afrika inavyo vyanzo toshelevu.



Huduma ya maji Njombe ilivyo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

MAZINGIRA

# Fedha za UVIKO-19 zilivyowatua ndoo wanawake vijijini Shinyanga

## •Hawaamini 'baibai' safari inayoanzia usiku

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

DUNIANI, maeneo mengi ya vijijini bado hayana huduma ya maji safi na salama, na wananchi wamekuwa wakitumia maji ambayo siyo salama kwa matumizi ya binadamu, yakiwemo ya kwenye, madimbwi na mabwawa ambayo pia huchangiwa na mifugo.

Sera ya Maji ya Mwaka 2002, inasema huduma ya maji inapaswa kufikia wananchi wa maeneo ya vijijini asilimia 85 na mijini asilimia 100, ifikapo mwaka 2020, ni miaka miwili sasa imepita, lakini bado kuna maeneo mengi vijijini haya huduma ya majisafi na salama na kuendelea kutumia maji machafu.

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA) ilipokea fedha za mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19, Sh.milioni 469 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria kwa wananchi.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akikagua mradi wa Maji katika kijiji cha Magwata Kata ya Kizumbi Manispaa ya Shinyanga utokanao na fedha za UVIKO-19, unaotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Shinyanga (SHUWASA), **PICHA: MARCO MADUHU.**

Mkurugenzi wa Mamlaka hiyo ya Maji Shinyanga (SHUWASA) Mhandisi Yusuph Katopola, anasema baada ya kupokea fedha hizo za UVIKO-19, ilibidi wazielekeze kwenye maeneo ambayo hayana kabisa huduma ya majisafi na salama, ili wamtue ndoo kichwani mwanamke.

Anataja maeneo ambayo walizielekeza fedha hizo za miradi ya majisafi na salama, kuwa ni kijiji cha Didia, Magwata, Bugwandege, Bugimbagu na Iselamagazi.

Anasema maeneo hayo waliyapendekeza, kwa sababu wananchi wake walikuwa wanapata shida ya kufuata majisafi na salama umbali mrefu, hususani wanawake ambao ndiyo waathirika wakubwa wakiteseka na ndoo za maji kichwani, ndipo wakaona wawatatulie shida hiyo.

"Miradi yote ya maji ambayo tumeitekeleza kupitia fedha za UVIKO-19 Sh.milioni 469 tulizopewa na Rais Samia Suluhu Hassani kupitia Wizara ya Maji, yote imekamilika na inatoa huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria," anasema Katopola.

Anawasisitiza wananchi kuwa kinachopaswa kwa sasa, ni kutuma maombi ya kuunganishiwa huduma ya maji majumbani mwao, ili wasichote maji tena kwenye vituo vya maji (maghati), bali wachote ndani ya makazi yao na kumtua ndoo kichwani mwanamke.

Meneja Usambazaji Maji kutoka SHUWASA, Mhandisi Uswege Mussa, anataja idadi ya wanufaika kwa kila mradi wa maji ambao wameutekeleza kwa kila kijiji: Didia watanufaika wananchi 3,700, Magwata wananchi 3,720, Bugwandege 6,900, Bugimbagu 1,179 na Iselamagazi 5,677.

**VIONGOZI WILAYA**

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anazungumzia dhana ya kumtua ndoo kichwani mwanamke, anasema dhamira ya serikali chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, haitaki kumuona mwanamke akibeba ndoo kichwani bali achote maji nyumbani kwake.

Anasema baada ya miradi hiyo ya maji kukamilika itokanayo na fedha za UVIKO-19, anatarajia kuona wananchi wakituma maombi kwa wingi kwenye Mamlaka hiyo ya Maji (SHUWASA), ili wavutiwe maji kwenye makazi yao, sababu mita zipo za kutosha 2,400 na huduma hiyo watauganishwa haraka sana.

"Kilichobaki sasa ni kwenu nyie wananchi kuomba kuunganishiwa huduma ya maji majumbani mwenu, ili kuiishi dhana kamili ya kumtua ndoo kichwani mwanamke," anafafanua Mboneko.

Anawataka pia wananchi waitunze miundombinu hiyo ya miradi ya maji na kuacha kuihujumu, ikiwamo kujiunganishia maji kinyemela kwa kutafuta mafundi wa mitaani maarufu 'vishoka', bali wafuate utaratibu ili miradi hiyo idumu muda mrefu kuwa hudumia.

Diwani wa Didia wilayani Shinyanga Richard Luhende, anashukuru eneo hilo kupata huduma ya majisafi na salama kutoka Ziwa Victoria, tatizo ambalo lilikuwa hitaji la wananchi kwa muda mrefu na lilikuwa likimsumbua wakati wa kampeni.

Anasema sasa hivi shida hiyo ya wananchi kudai huduma ya majisafi na salama imeshakwisha, na wanachokifanya kwa sasa ni kuhamasisha watume maombi ya kuunganishiwa huduma ya maji hayo majumbani mwao.

Mwenyekiti wa kijiji cha Didia wilayani Shinyanga, Mrisho Hamadi, anasema eneo hilo lina jumla ya wakazi zaidi ya 4,000, na walio omba huduma ya kuunganishiwa maji majumbani mwao hadi sasa ni Kaya 94.

"Idadi wananchi 94 kuomba kuunganishwa maji majumbani mwao ni ndogo ikilinganishwa na Kaya tulizonazo zaidi ya 4,000, hivyo tunarajia sisi kama viongozi kwa kushirikiana na Diwani tuitishe mkutano wa hadhara, na kutoa elimu kwa wananchi wajitokeze kutuma maombi ya kuvutiwa maji," anasema Hamadi.

**MKAZI MNUFAIKA**

Ashura Masanja mkazi wa kijiji cha Magwata ambaye ni miongoni mwa wanufaika wa miradi hiyo ya Majisafi na salama kupitia fedha za UVIKO-19, anasema kwa sasa wameondokana na shida ya kupoteza muda wa kufanya shughuli za maendeleo sababu ya kufuata maji umbali mrefu.

Anasema, awali walikuwa wakiteseka kufuata huduma ya majisafi na salama katika vijiji jirani, na wao wanawake ndiyo walikuwa wakitaabika sana kufuata maji hayo, na wanapochelewa kurudi huingia migogoro na waume zao na kuziweka ndoa zao matatani.

"Tunaishukuru sana Serikali kwa kusikia kilio chetu sisi wanawake wa kijijini na kututua ndoo kichwani, sasa hivi maji yapo hapa jirani, na maji haya lazima tuyavute majumbani mwetu, na itabaki kuwa historia kwamba tulikuwa tukiamka usiku kufuata maji umbali mrefu," anasimulia Ashura.

Samsoni Paulo mkazi wa kijiji cha Bubale wilayani Shinyanga, anasema suala la kusomba maji majumbani ni jukumu la mwanamke, lakini huwa inafikia kipindi anamhurumia mkewe anayefuata maji umbali mrefu, na kuamua kumsaidia kwa kutumia usafiri wa baiskeli, hivyo anaishukuru serikali kwa kuwatatulia changamoto hiyo.



Hali halisi ya shida ya maji mkoani Shinyanga, ambayo inafanyiwa kazi sasa. **PICHA; MAKTABA.**



## Waziri aagiza mikopo itolewe kwa wavuvi

**Na Magdalena Jackson (SJMC)**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameitaka wizara hiyo kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) kutekeleza kwa haraka utoaji mikopo kwa wavuvi.

Agizo hilo linakuja baada ya kutengwa Sh. bilioni 60 kwa mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya wavuvi kupitia vyama vya ushirika, vikundi vya wavuvi, vikundi vya wakuzaji viumbe maji, vikundi binafsi na kampuni za wavuvi.

Ndaki aliagiza hayo juzi kwenye hafla ya kutia saini mkataba wa utekelezaji wa mradi wa ununuzi wa boti za uvuvi na vizimba vya samaki iliyofanyika jijini hapa.

Alisema mkopo huo hauna riba, hivyo ni nafasi ya pekee kwa wazalishaji wa samaki kuongeza uzalishaji kupitia mikopo hiyo ambayo itahusisha zana za kisasa za uvuvi zikiwamo boti, nyavu, vifaranga vya samaki, injini, vizimba na pembejeo za wakulima wa mwani.

Alisema hali hiyo itasaidia kuongeza uzalishaji wa samaki kutoka tani 497,567 zinazozalishwa kwa mwaka nchini, uzalishaji ambao haukidhi mahitaji katika viwanda na matumizi ya chakula.

Alisema wavuvi na wakuzaji viumbe maji wachangamkie fursa hiyo ambayo imetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan ili kunufaika nayo.

Alizitaka halmashauri kuwahamasisha wananchi kushiriki kwa wingi na kuwa waaminifu katika kurejesha mikopo hiyo.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema wizara itahakikisha inasimamia ukopeshaji wa wavuvi wadogo na wa kati na kuwasaidia vijana kujiajiri wenyewe kupitia ufugaji wa samaki na kuongeza uzalishaji ili walengwa waliokusudiwa, wapate mikopo hiyo.

Alisema serikali imetoa Sh. bilioni 100 kwenye Wizara ya Mifugo ambapo Sh. bilioni 60 ni kwa upande wa uvuvi na Sh. bilioni 40 kwa ajili ya sekta ya mifugo.

"Benki ya Maendeleo inayo kazi kubwa kuhakikisha mikopo inakwenda kwa walengwa kwa sababu watu wengi wamekuwa wakilalamika kuhusu mchakato mrefu wa kupata mikopo hiyo, hivyo benki wanapaswa kuwa wabunifu ili kuendana na kasi ya kuwafikia wananchi kwa urahisi," alisema.

Dk. Christine Ishengoma, Mwenyekiti Kamati ya Bunge Kilimo, Mifugo na Maji, alisema kamati inaamini kupitia mikopo hiyo na zana za uvuvi, upatikanaji wa samaki utaongezeka kwa wingi kwa wavuvi kuongeza kipato.

Alisema kamati itaendelea kusisitiza upatikanaji wa mikopo zaidi kwa wavuvi kutoka katika Benki ya Maendeleo ya Wakulima na kufuatilia utekelezaji na upatikanaji wa fedha katika miradi hiyo.

Mkurugenzi wa TADB, Frank Nyabundege, alitaja baadhi ya malengo ya benki hiyo kuwa ni pamoja na kuchangia utoshelevu wa chakula na usalama endelevu wa chakula nchini na kusaidia mapinduzi ya kilimo.

"Benki ya Maendeleo ya Kilimo imejikita katika sekta zote tatu yaani kilimo, ufugaji na uvuvi, hivyo imewekeza Sh. bilioni 5.3 katika uvuvi wa vizimba ili kuhakikisha uwekezaji mkubwa wa uvuvi nchini," alisema.

# Bunge: Serikali sasa itekeleze mradi Liganga na Mchuchuma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeagiza serikali kuanza kutekeleza mradi wa Liganga na Mchuchuma na kulipa fidia wananchi waliopitiwa na mradi huo.

Akitoa maelekezo hayo jana baada ya kikao na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Kihenzile, alisema mradi huo umekuwa na miaka 124 iliyopita na umekuwa ukiimbwa bila kutekelezwa.

"Mradi huu sasa uanze na tumeelekeza wananchi walipwe fidia, mwaka huu walipanga kufanya uhakiki ili baadaye waanze kulipa, sasa tumewashauri tu ikiwezekana ifikapo Desemba, serikali itafute namna ya kupata fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi kwa sababu kwa muda mrefu wananchi hao wamehifadhi hayo maeneo," alisema.

Kiongozi huyo alisema dhamira ya kamati ni kuona miradi hiyo sasa inaanza kutekelezwa.

Alisema serikali inatekeleza miradi ya kimkakati 17 ambapo mitatu ipo kwenye kamati hiyo, ukiwamo mradi huo, pia kuna mradi wa magadi soda mkoani Arusha na mradi wa eneo huru la kibiashara wa Bagamoyo.

Alipoulizwa kuhusu kauli ya kamati kuhusu kupanda kwa bei ya bidhaa mbalimbali, Kihenzile alisema suala hilo halikuwa sehemu ya mjadala wao lakini wabunge wameshauri serikali iweke mikakati ya kushusha bidhaa za vitu ili kuwasaidia wananchi.

Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaudi Kigahe, alisema wizara imewasilisha taarifa ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati mitatu kwa kamati hiyo, ukiwamo Liganga na Mchuchuma.

"Msisitizo wa kamati ulikuwa wa Mchuchuma na Liganga ambao ni wa muda mrefu na tunaona sasa ni muda mwafaka kutekeleza mradi huu ili tukipata chuma hapa nchini bei iwe chini na kuongezea wananchi kipato,"alisema.

Naibu waziri huyo alisema wanaangalia namna ya kulipa fidia kwa wananchi wa Ludewa na kupata mwekezaji mahiri awekeze ili kuendeleza mradi huo. "Kuhusu magadi soda, tumekamilisha taratibu zote, kwa sasa tunafanya taratibu za kupata hati ya eneo lile lakini tutatangazia wawekezaji kuwekeza kwenye eneo lile,"alisema.

Pia alisema eneo la uwekezaji la Bagamoyo bado wanapitia upya mpango wake ili kuona namna ya kumalizia kulipa fidia na kupata mwekezaji ambapo eneo walilokusudia ni la Bandari ya Bagamoyo.



Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara mkoani Kagera wakiingia bungeni kwa ajili ya kukutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Soko latengeneza hasara bilioni 1.2/-

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kipindi cha miezi minane Soko Kuu la Majengo jijini Dodoma limetengeneza hasara ya Sh. bilioni 1.2 kutokana na uongozi wa jiji hilo kulazimisha magari ya ndizi, viazi na matunda kushusha mizigo kwenye Soko la Job Ndugai.

Mwenyekiti wa Soko la Majengo, Godson Rugazama, alibainisha hayo jana katika mkutano mkuu wa wafanyabiashara wa soko hilo.

Alisema katika kipindi hicho, soko hilo limetengeneza hasara hiyo kutokana na uongozi wa jiji kupiga marufuku ushushaji wa mizigo kwenye soko hilo kama ilivyokuwa awali.

Rugazama alisema uongozi wa jiji ulipiga marufuku mwaka jana ushushaji wa mizigo hiyo kwa madai kuwa unataka Soko la Job Ndugai kuchangamka kibiashara baada ya kuona kuwa hakuna wafanyabiashara katika eneo hilo.

"Hivi sasa tangu kupiga marufuku ya ushujaji wa mizigo katika soko hili, wafanyabishara wa Soko la Majengo tunalazimika kukodi magari madogo na washushaji wa mizigo ili kuleta hapa.

"Hii hoja ya kusema kuwa kushusha mizigo yetu Soko la Job Ndugai kutasaidia kuchangamsha biashara ni hoja mfu, tena inatupa hasara kubwa sana sisi wafanyabiashara. Tunaomba uongozi wa jiji kupitia baraza la madiwani kuifanyia kazi haraka ili tupate suluhu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema hivi sasa magari sita ya ndizi na 10 ya matunda yalazimika kwenda Soko la Job Ndugai kwa ajili ya kushusha mizigo ambayo ikishashushwa huko, wafanyabiashara wanalazimika kukodi magari madogo ili kupeleka bidhaa Soko la Majengo.

"Katika magari hayo sita ya ndizi mfanyabiashara analazimika kukodi kirikuu nne hadi tano, kwa kila moja ni Sh. 40,000, bado gharama za washushaji na wapakiaji, ukipiga hesabu kwa kila siku kama 240,000, ukijumlisha mara hiyo miezi minane ni zaidi ya Sh. bilioni 1.2, hasara ambayo tumekuwa tukitengeneza," alifafanua.

Vilevile, alisema kupitia risala yao kwa uongozi wa jiji, wamependekeza utaratibu wa zamani wa kushusha bidhaa zao sokoni hapo urudishwe.

"Soko la Job Ndugai halikuanzishwa ili kuua mitaji ya wafanyabiashara wengine. Kama wanataka kulifanya Soko la Ndugai kufanya biashara, basi watafute njia nyingine siyo kulitumia Soko la Majengo kuimarisha Ndugai," alisema.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Ofisa Masoko wa Jiji hilo, Getrude Lumambo, alisema hoja zote amezipokea kwa niaba ya mkurugenzi na atazifikisha sehemu husika kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za CAG kwa mwaka 2020/21, pamoja na mambo mengine, imenyooshea kidole hasara ya mabilioni inayopata serikali kutokana na masoko iliyoyajenga kutotumika ipasavyo.



# Madiwani wabaini tatizo katika ruzuku pembejeo

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wameiomba serikali kuingilia kati uandikishwaji wa wakulima kwa ajili ya utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo, wakidai kuna sintofahamu.

Akizungumza jana kwenye kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Diwani wa Kata ya Serengeti Martin Mwainyekule, alisema licha ya serikali kutangaza wakulima wote waandikishwe ili kupatiwa ruzuku ya pembejeo za kilimo, hali ni tofauti katika halmashauri hiyo.

Alisema kuwa baada ya serikali kutangaza wakulima waandikishwe, kazi ilianza kwa kasi lakini baadaye ikasitishwa na mpaka sasa wananchi hawajui kinachoendelea.

Diwani huyo alisema asilimia 70 ya wananchi wa wilaya hiyo ni wakulima, hivyo kusuasua kwa uandikishwaji kwa ajili ya kupata pembejeo za kilimo kwa msimu ujao kumeleta wasiwasi miongoni mwa wakulima na sasa wanaiomba serikali kuingilia kati ili kazi hiyo ikamilike na wakulima waanze kuigizwa kwenye utaratibu wa kupata mbolea.

"Huko mtaani wakulima wanalalamikia uandikishwaji kwa ajili ya kupata pembejeo, sasa sijui kuna upendeleo. Tunaomba viongozi kuingilia kati jambo hili maana tayari wameingia hofu kwamba huenda hawana sifa ya kuingia kwenye utaratibu huo, tunakosa majibu ya kuwapatia kwa sababu hatujui nini kinaendelea," alisema Mwainyekule.

Pia aliwaomba viongozi wa halmashauri kununua silaha kwa ajili ya kupambana na ngedere ambao wamekuwa wakivamia mashamba ya wakulima na kuharibu mazao.

Alisema hadi sasa wanaona hakuna utekelezaji wa jambo hilo licha ya taarifa kutolewa kwenye baraza lililopita juu ya hatua za kukabiliana na wanyama hao ambao wamekuwa wakisababisha hasara kubwa kwa wakulima.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Ismail Mlawa, alisema tayari silaha zimekwishanunuliwa na kinachosubiriwa ni utelezaji wa kuwaondoa ngedere kwenye mashamba.

Aliwatoa hofu wakazi wa Wilaya ya Kyela juu ya wanyama hao waharibifu na kuwaomba kutoa taarifa kwenye vyombo vya usalama ili kujua namna ya kukabiliana na wanyama hao.

Akizungumzia suala la uandikishwaji wa pembejeo kwa wakulima, mkuu wa wilaya alisema kazi hiyo imesuasua kutokana na sensa ya watu na makazi, hivyo baada ya kukamilika kwa sensa, itaendelea kama kawaida na wakulima wote watafikiwa.

Alifafanua kuwa wakulima watakaoandikishwa ni wale wenye mashamba na wanaofanya shughuli za kilimo wilayani Kyela na mkulima yeyote mwenye shamba nje ya wilaya hiyo atalazimika kujiandikisha eneo liliko shamba lake.

"Sensa ya watu na makazi imesababisha uandikishwaji wa wanufaika wa pembejeo kusuasua lakini baada ya zoezi la sensa kukamilika litaendelea na kuwafikia wakulima wote, lakini ninaomba nitoe ufafanuzi kwamba wakulima watakaoandikishwa ni wale wote ambao wana mashamba hapa wilayani Kyela tu, hivyo kama mashamba yako yako nje ya wilaya hii utajiandikisha yaliko," alisema Mlawa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Katule Kingamkono, alisema kila mkulima mwenye kigezo, atapata pembejeo za kilimo.

Aliwaomba waratibu wa kazi hiyo kuwa waaminifu kwa kuhakikisha kila mkulima anayestahili apatiwe mbolea kwa bei elekezi ya serikali na kumwezesha kupata mavuno mengi.




Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua (wa pili kushoto), akipokea zawadi kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kutoka kwa Mkurugenzi wa Hazina na Masoko ya Mitaji wa Benki ya Azania, Gilbert Mwandimila, katika hafla ya chakula cha jioni kwa ajili wadau mbalimbali na viongozi wa serikali, jijini humo juzi, kwa lengo la kujua huduma mbalimbali zinazotolewa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Milioni 65/- zatengwa ujenzi soko la kisasa

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya imetenga Sh. milioni 65 kwa ajili ya ujenzi wa soko la kisasa la Orofea katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Katule Kingamkono, fedha hizo zimetolewa kupitia mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Alisema jana kuwa soko jipya litakalojengwa, litasaidia kukidhi mahitaji ya wananchi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kyela ambao wanakosa mahitaji muhimu ndani ya soko lililopo sasa.

Mwenyekiti huyo alisema halmashauri imetoa Sh. milioni 65 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa soko jipya. Kati ya fedha hizo, Sh. milioni 15 zitatumika kwenye ujenzi wa vyoo, Sh. milioni 15 zitaboresha huduma zingine.

"Tayari fedha ipo, kinachosubiriwa ni kuanza utekelezaji wa ujenzi wa soko kubwa la kisasa ambalo litakidhi mahitaji ya wana Kyela, tunaamini soko hilo litakuwa na miundombinu yote muhimu ikiwamo barabara, vyoo na huduma zingine," alisema Katule.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, alisema ujenzi wa soko hilo utakamilika ndani ya muda uliopangwa ili lianze kutoa huduma.

Alisema atahakikisha soko hilo linajengwa katika viwango vinavyotakiwa kulingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Mkurugenzi huyo alilipongeza baraza la madiwani kwa kuibua ujenzi wa miradi mbalimbali kwa ajili ya kuwanufaisha wananchi.

Alibainisha miradi inayoendelea inajumuisha ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika Hospitali ya Wilaya ya Kyela na vituo vya afya vinne.

# DC alia na tangawizi Rungwe kukosa soko

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

SERIKALI wilayani Rungwe Mkoa wa Mbeya imekiri kukosekana kwa soko la uhakika la tangawizi, hivyo kulazimika kusaka wawekezaji wadogo wa viwanda vya kuchakata na kusindika kutoka ndani na nje ya nchi, hususani Zambia na Malawi.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anne, jana alisema uzalishaji wa tangawizi wilayani humo ni mkubwa kulinganisha na mahitaji, hali inayosababisha wakulima kuuza kwa bei ya hasara.

Alisema kutokana na hali hiyo, wameanza kutengeneza mazingira rafiki kwa ajili ya kuwavutia wawekezaji kusindika na kuongeza thamani bidhaa hizo na kuwasaidia wakulima kuuza kwa watu hao.

Alisema mikakati mingine ni kuendelea kusaka masoko nje ya nchi kama vile Malawi, Zambia na Afrika Kusini ambao walitangaza nia ya kununua bidhaa hiyo ambayo inazalishwa kwa wingi wilayani Rungwe.

"Tumeona tatizo lililopo kwa wakulima wetu ni kukosa soko la uhakika la bidhaa hiyo na kusababisha kuuza kwa bei ya hasara licha ya kutumia gharama kubwa kwenye uzalishaji," alisema Dk. Anney.

Mkulima wa tangawizi, Azamela Braison, alisema kuwa hali ya biashara ni mbaya na kuna hofu mali zao kutaifaishwa kutokana na mikopo ambayo ilitumika kama mitaji katika uzalishaji.

"Tumezalisha kwa wingi tangawizi lakini hakuna soko la uhakika, tunalazimika kuuza kiholela kwa bei ya Sh. 500 mpaka Sh. 1,000 lakini hakuna faida yoyote maana tunategemea wasafiri katika barabara yetu ya Mbeya-Kyela hadi mpaka wa Boda Kasumulu," alisema Braison.

Wakati wakulima na wachuuzi wa zao la tangawizi wilayani Rungwe wakilalamikia kukosekana kwa soko la uhakika, hali ni tofauti kwa wafanyabiashara wa Jiji la Mbeya ambao wanachukua bidhaa hiyo wilayani Rungwe na kuuza sokoni kwa bei ya kuanzia Sh. 200 kwa hadi 500 kwa tangawizi moja kulingana na ukubwa.

Stella John, mmoja wa wafanyabiashara hao, alisema wanapata faida kwa kuwa anaponunua kwa ujazo wa kipimo maalum cha Sh. 2,000 kwa mkulima na akiingiza sokoni anapata faida ya Sh. 5,000, lakini kulingana na ukubwa wa kila tangawizi.



## Mwinyi azipongeza taasisi uimarishaji huduma za jamii

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amesema ushiriki wa taasisi zisizo za kiserikali katika uimarishaji wa huduma za kijamii ni muhimu kwa kuzingatia serikali haina uwezo wa kuwafikia wananchi wote.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na viongozi wa Taasisi za Milele Zanzibar Foundation na IFRAJ waliofika kumsalimia pamoja na kuelezea shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hizo.

Alisema kwa kipindi kirefu sasa taasisi hizo zikifanya kazi kubwa ya kuisaidia serikali, hususan katika uimarishaji wa sekta za huduma ya jamii.

Alizipongeza taasisi hizo kwa kufanya kazi kubwa na kuwa taasisi zinazofanya vyema zaidi hapa nchini katika kuisaidia serikali uimarishaji wa sekta za huduma za jamii, ikiwamo afya, elimu, maji na uwezeshaji wajasiriamali.

"Ninaridhika na kazi kubwa mnayofanya kwa kuwa inagusa vipaumbele vya serikali katika kuimarisha huduma za jamii," alisema.

Alifurahishwa na kazi kubwa inayofanywa na taasisi hizo katika kujenga mifumo pamoja na kuzingatia umuhimu wa ujenzi wa miundombinu, uwepo wa rasilimali watu na mahitaji ya vifaa katika sekta hizo.

Dk. Mwinyi alisema Zanzibar inakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa majisafi na salama na hatua inayochukuliwa na taasisi hizo ya kusaidia upatikanaji wa pampu pamoja na uchimbaji wa visima ni ya kupongezwa.

Naye Mkuu wa Miradi wa Taasisi ya Milele Zanzibar Foundation, Khadija Ahmeid Sharrif, alisema taasisi hiyo ipo mstari wa mbele kuisaidia jamii kupitia sekta mbalimbali.

Kwa upande wake, Meneja wa Taasisi ya IFRAJ, Abdalla Said Abdalla, alisema taasisi hiyo inajishughulisha na ujenzi wa nyumba za makazi kwa wananachi wenye kipato cha chini na sasa wanakamilisha ujenzi wa nyumba 500 zinazogharimu zaidi ya Sh. bilioni 7.5.

# Mtoto aliyeokolewa kwenye moto na bibi aendelea vizuri

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NADIL Issa (5) ambaye amenusurika kifo baada ya bibi yake kuruka naye kutoka ghorofani kutokana na nyumba yao kuungua moto, anaendelea vyema na matibabu.

Bibi wa mtoto huyo Rehema Chande (70), alipoteza maisha eneo la Mkunazini Mjimkongwe Zanzibar, baada ya kuanguka kutoka ghorofani akijiokoa yeye na mjukuu wake baada ya nyumba yao kuungua.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Muuguzi katika wodi ya watoto hospitalini hapo, Thuwaiba Said, alisema hali ya mtoto huyo inaendelea vizuri na hakupata majeraha makubwa. Muuguzi huyo alisema, mtoto huyo alifikishwa hospitali hapo juzi majira ya saa saba mchana na kuanza kupatiwa matibabu.

"Mtoto tulimpokea majira ya saa saba mchana Jumanne kutokana na majeraha aliyoyapata baada ya bibi yake kujirusha ghorofani akijiokoa na moto uliozuka katika nyumba wanayoishi," alisema.

Alisema mtoto amefanyiwa vipimo vyote hakukutwa na majeraha makubwa kutokana na kuangukia kifuani kwa bibi yake.

Mama wa mtoto huyo, Hawa Kundi Haji, alisema alipigiwa simu na majirani wa mkwe wake (marehemu) kuwa amefariki dunia na mtoto wake amepelekwa hospitali.

"Baada ya kupata taarifa nilipatwa na mshtuko mkubwa na kulazimika kukimbilia hospitali, hata hivyo nashukuru kukuta hali ya mtoto wangu sio mbaya ingawa nina majonzi ya kumpoteza bibi yake ambae ndiye alikuwa mlezi wake," alisema.

Alisema mtoto wake alikuwa akiishi na bibi na baba yake ambaye waliachana na kila mmoja kuishi eneo lake.

Baba wa mtoto huyo, Issa Ramadhan Ismail, alisema wakati tukio la moto linatokea hakuwapo nyumbani na alipokea taarifa kwa mshtuko mkubwa. Aliiomba serikali na watu mbalimbali kumsaidia kwa sababu hakuna kitu kilichookolewa katika nyumba yao baada ya kuteketea kwa moto.

"Tukio hili sitaweza lisahau maishani mwangu, kwanza nimepoteza mama yangu mzazi, mtoto wangu amepata majeraha na hapa unapotuona hatuna hata nguo ya kuvaa zaidi ya hizi tulizovaa mwilini kwa sababu hakuna kitu kilitoka ndani ya nyumba vyote vimeungua," alisema kwa masikitiko.

Alisema baada ya ndoa yake kuvunjika, mtoto wake Nadil akiwa na umri wa miaka miwili, alilelewa na bibi yake kumpunguzia mzigo wa malezi mtalaka wake.

Alisema ingawa walikuwa wakiishi pamoja na mama yake, lakini muda mwingi mtoto alikuwa na bibi yake na huko hospitali anamtaja bibi yake mara kwa mara.

**WAZIRI AZUNGUMZA**

Akizungumza baada ya kumkagua mtoto Hospitali, Waziri wa Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe, alisema Rehema (marehemu) anahitaji kupewa nishani ya ushujaa kwa kumuokoa mtoto huyo katika tukio la ajali ya moto.

"Kwa kweli tukio hili ni la kusikitisha, lakini bi Rehema licha ya kufariki dunia ni shujaa kwa kujitoa muhanga kwa kumuokoa mjukuu wake...ndiyo wazazi tunavyokua hasa mzazi wa kike," alisema.

Alisema wanawake ndiyo walezi wakuu wa watoto na wapo tayari kujitoa muhanga ili kunusuru maisha ya watoto kama kitendo alichokifanya bi Rehema.

Alitoa pole kwa familia hiyo kwa kuondokewa na mpendwa wao na kuwataka kuwa na subira katika kipindi hiki kigumu cha msiba huo.



Waziri wa Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe, akimjulia hali mtoto, Nadil Issa, aliyenusurika kifo baada ya bibi yake kuruka naye kutoka gorofani wakati akijihami dhidi ya moto kwenye nyumba wanayoishi eneo la Mji Mkongwe, akiwa anaendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kampuni za teknolojia zaanza uwekezaji Z'bar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imezindua mpango wa kuvutia na kukaribisha kampuni za teknolojia visiwani humo huku kampuni ya Masoko inayokua kwa kasi barani Afrika ikifungua ofisi ya kwanza Zanzibar.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa mpango huo wa kituo cha biashara cha Pavillion katika Mji wa Fumba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji Mudrik Ramadhan Soraga, alisema utekelezaji wa mpango huo utasaidia kukuza matumizi ya teknolojia na kukuza uchumi wa taifa na ajira kwa vijana.

Waziri Soraga alisema,kampuni za teknolojia hazitahitaji tena kufungua ofisi na kuhamisha watu wao kwenda Dubai au London kusimamia shughuli zao barani Afrika.

"Tunatoa mazingira ya wazi na wezeshi kwa makampuni yote ya teknolojia na washiriki wa timu zao kuwa mjini Zanzibar mojawapo ya maeneo yanayovutia zaidi duniani kuruhusu kila mtu anayefanya teknolojia kwa ajili ya Afrika kuwa na msingi barani humu," alisema.

Alisema kampuni ya Silicon Zanzibar inaunga mkono sera ya serikali ya Uchumi wa Buluu ili kukuza maendeleo ya kiuchumi kwa kupitia chini ya mazingira na mahitaji ya rasilimali endelevu.

Alisema wafanyabiashara wa kiteknolojia wana uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi hasa kiuchumi kwa vile hawategemei hali ya hewa, jambo ambalo litaisaidia Zanzibar kuinua uchumi wake dhidi ya sekta za msimu kama kilimo na utalii.

Alisema tukio hilo ni la kihistoria kwa Zanzibar na ndiyo kituo cha kwanza baada ya kuweka mkakati wa kuanzisha mpango maalum wa kualika kampuni za teknolojia kutoka nchi mbalimbali duniani kuwekeza visiwani humo.

Aidha, alisema lengo la mpango huo ni kuruhusu shughuli za uwekezaji kuendelea kuchukua nafasi kwa kukaribisha kampuni mbalimbali kutoa huduma ikiwamo za vyakula na matumizi mengine ya nyumbani kwa wakazi wa eneo hilo ili kupatikana kwa karibu zaidi. Waziri Soraga alisema uwekezaji katika teknolojia unakwenda sambamba na sera ya serikali ya uchumi wa buluu na kila sekta inayoguswa ni suala la mifumo ili kuvutia wawekezaji.

Hata hivyo, alisema mtazamo wa serikali kwa sasa ni uwekezaji katika nyanja zote na kwamba ni vyema kuangalia zaidi fursa zilizo katika eneo hilo ikiwamo za sekta ya uchumi wa buluu katika kutumia rasilimali zilizomo kwa kuzingatia uchumi endelevu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya uhandisi ya CPS, Sebastian Dietzold, alisema CPS inasaidia kuendeleza jumuiya zenye nguvu zinazoongeza thamani kwa wawekezaji kama Wasoko, kwa madhumuni ya msingi ya kuwawezesha watu wa Zanzibar na wafanyabiashara.

"Silicon Zanzibar tayari imevutiwa na kampuni ya Wasoko kama mshirika wake wa kwanza, ni kampuni inayokua kwa kasi barani Afrika kama inavyotambuliwa na Financial Times, imetangaza kufungua kituo kipya katika Mji wa Fumba sambamba na kuwatumia zaidi ya wafanyakazi 40 wa teknolojia na viongozi wakuu akiwamo Mkurugenzi Mtendaji wa Wasoko, Daniel Yu," alisema Sebastian. Alisema kampuni yao inaongeza thamani kwa jumuiya za wawekezaji wa ndani na nje na imani yake kwamba kituo hicho kitaongeza uwekezaji na thamani ya mji huo wa kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Sharif, aliahidi kwamba ZIPA itaendelea kutoa ushirikiano ili lengo la kuanzishwa mradi huo linatimia kwa sababu wawekezaji hao wanaisaidia serikali katika kuinua uchumi wa nchi.

Aliwapongeza wawekezaji hao kwa kutumia teknolojia ya kusambaza bidhaa madukani ikiwamo vyakula kwa sababu wakazi zaidi ya 500 wanaokaa katika mji huo watapata fursa ya teknolojia hiyo kwa kupatiwa bidhaa wanazozitaka.

Eneo la uwekezaji Fumba town limeshajengwa nyumba 234 na lina zaidi ya wakazi 500 hadi sasa, mpango wa Zanzibar Silicon utaruhusu uwekaji wa maduka na huduma muhimu.

TANGAZO


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KARIAKOO**
**POPOTE ULIPO**
**Ndugu, BURGIS LIMITED**
**WITO WA KUITWA SHAURINI**
**KESI YA MADAI 256 NO 2021**
**MDAI BURGIS LIMITED**
**MDAIWA: EDENUILLE INTERNATIONAL TANZANIA**

Unaamriwa na mahakama ya mwanzo kariakoo kuja kusikiliza shauri la madai ya **19,627,200/= No 256121** siku ya **JUMATANO** tarehe **14/9/2022 saa 2:30 ASUBUHI**, **KAMA HUKUHUDHURIA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA.**
**AMRI HII IMETOLEA LEO TAREHE 31/8/2022**


HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
KARIAKOO - ILALA
DAR-ES-SALAAM

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH JOHN MAKELELE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.4733-0019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ST. MARGARET MARIA ALAKOK GIRLS SECONDARY SCHOOL** mwaka 2014. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/344453/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JEMA EDSON** anatangaza kupotelewa na cheti cha **UALIMU kozi ya UALIMU DARAJA B** chenye namba ya usajili E.518/43 kilichotolewa na chuo cha **NDALA TEACHER'S COLLEGE** mwaka 1996, yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **MIN/RB/685/2016**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**KAHAMA SDA PRE AND PRIMARY SCHOOL** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 276 DHL.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI
**KAH /RB/ 584/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SUZANA MESHACK NFOJE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CROWN** yenye usajili namba **T515 DPP , CHASSIS NAMBA: GRS1805003620** na **ENGINE NAMBA: 4GR0010834.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: DAR/BUG/RB/343728/2022**

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT TANGA**
**BILL OF COSTS No. 17/2022**
**(Originating from Misc. Civil Cause No. 48/2021)**

**WAREHEMA KIBAHA-ADVOCATE**
**(Interim liquidator)......................................D/HOLDER**
**VS**
**MIKE WILHELM KITWAKA (Petitioning under Power of Attorney Floyd Vernon hammer) ......J/DEBTOR**

**TO:**
**MIKE WILHELM KITWAKA (Petitioning under Power of Attorney Floyd Vernon Hammer)**

**NOTICE OF MENTION**

**TAKE NOTICE** that on the 7TH SEPTEMBER, 2022 at 09:00 O'clock in the forenoon the application has been fixed for **MENTION FOR NECESSARY ORDERS Before Hon. B.R NYAKI, DR**
**ALSO TAKE NOTICE** that in default of your appearance on that date the case will be heard and determined in your absence.
GIVEN under my hand and seal of the Court this 16TH AUGUST, 2022.

DEPUTY REGISTRAR
TANGA

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISAYA INNOCENT NATAI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5290/0063** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya CHRISTON BOYS mwaka 2021,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/KIJ/RB/342187/2022**

## KUPOTEA KWA PASIPOTI YA KUSAFIRIA



**JOAS MUGANYIZI ZACHWA** anatangaza kupotelewa na pasipoti ya kusafiria yenye namba **TAE029034** iliyotolewa na wizara ya mambo ya ndani **UHAMIAJI** mwaka 2018,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/345639/2022**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI WA KIWANJA

**Nkwangu Luhende** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanda Namba **475 kitalu "MM"** kilichopo Lubaga Manispaa ya Shinyanga.
Kwa yeyote atakaiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo Karibu au awasiliane na Nkwangu Luhende kwa simu namba **0788908603**
**Rbnamba:SHI/SHI/RB/344187/2022**

Musa Makungu
AFISA ARDHI
MANISPAA YA SHINYANGA

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

# OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676




**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Biden azindua kampeni uchaguzi wa wabunge

**WASHNTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden miezi miwili kabla ya uchaguzi wa bunge nchini humo amezindua kampeni ya wabunge huku akiwatupia lawama wafuasi wa Donald Trump kwa kuunga mkono ghasia za kisiasa.


Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa jana na RFI, wiki iliyopita, Joe Biden alifananisha itikadi ya Donald Trump kama itikadi za 'kifashisti'. Taarifa hiyo ilisema katika mkutano wa hadhara alioufanya Rais huyo mwanzoni mwa wiki hii huko Pennsylvania, alikwenda hatua moja zaidi na kuwashambulia wafuasi wa Trump juu ya mizozo yao ya kisiasa, na kwa upande mmoja hotuba ya uungaji mkono usio na kikomo kwa polisi na kuhusu shtuma kwa washambuliaji wa makao makuu ya Bunge la Marekani.

"Mpo upande gani, 'Make America Great Again' huwezi kuwa mshirika wa polisi na mshirika wa uasi, acha niseme hivi kwa marafiki zangu 'Maga Republicans' wanaoshiriki vikao vya Baraza la bunge la Congress, usiniambie unaunga mkono vikosi vya usalama ikiwa hutakemea yaliyotokea Januari 6, 2021" alisema.

Wakati huo huo Biden alishutumu mashambulizi makali ya kambi ya wahafidhina dhidi ya FBI tangu msako kwenye klabu ya kibinafsi ya Donald Trump iliyoko Florida, huku alieleza kuwa suala hilo linachukiza.

Pia inaelezwa kuwa Joe Biden ana shauku ya kuonyesha kuwa yuko nyumbani, karibu na Scranton, mji wake kwasababu ni katika mji ambapo Trump atafanya mkutano Septemba 2 mwaka huu.

Taarifa ya RFI ilibainisha kuwa Rais huyo wa zamani atashiriki jukwaa na mgombea wake wa ugavana wa jimbo hilo muhimu, mtu ambaye anatajwa kuwa alikuwa mstari wa mbele kati ya waandamanaji huko Washington Januari 6, 2021.





Mawakili James Orengo, Paul Mwangi, Philip Murgor na Julie Soweto wakiwasilisha hoja zao katika mahakama ya juu dhidi ya pingamizi la kura za uchaguzi wa urais nchini Kenya. **PICHA MTANDAO.**

# Kesi pingamizi la urais Kenya yazidi kurindima

**NAIROBI,** KENYA

WAKILI katika timu ya wanasheria wa kiongozi wa Azimio Raila Odinga Julie Soweto, amedai kuwa kura 4,463 zilitolewa kutoka kwa mteja wake na kuongezwa kwa Rais mteule William Ruto katika Kaunti za Bomet, Kiambu, Kakamega, Nairobi na Baringo.

Akizungumza katika mahakama ya Juu nchini Kenya jana Julie, alilalamika kwamba kulikuwa na tofauti katika fomu 41 za 34A kutoka Bomet, Kiambu na Kakamega zilizopewa maajenti na zile zilizopo kwenye tovuti ya Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), ambazo ziliwasilishwa katika kituo cha kitaifa cha kujumlisha kura cha Bomas.

"IEBC ilinunua seti mbili za fomu 34A licha ya kutakiwa kununua kijitabu kimoja pekee ambacho kingetumiwa katika vituo vya kupigia kura huku 2/2 kikihifadhiwa kwenye bahasha isiyoweza kuguswa, hati ya kiapo ya Celestine Anyango inaonyesha ubaya wa kimakusudi katika matumizi ya fomu.

"Fomu ambazo mawakala wanazo na fomu kwenye tovuti ni sawa katika vipengele vyote namba za mfululizo, mihuri na sahihi, hata hivyo, takwimu katika fomu zimebadilishwa na ni tofauti," alisema.

Wakili Mkuu James Orengo, ambaye pia katika timu ya wanasheria wa Odinga, alidai kuwa IEBC haina utendakazi na haiwezi kufanya uchaguzi, huku akidai kuwa fomu hizo zilibadilishwa.

> **"Baada ya kutathmini uwazi wa kura hiyo, itabainisha iwapo William Ruto amefikia kiwango cha kikatiba cha asilimia 50 pamoja na kura moja kutangazwa kuchaguliwa katika duru ya kwanza," alisema.**

**AGIZO KURA KUHESABIWA UPYA**

Katika hatua nyingine Mahakama ya Juu iliiamuru tume ya uchaguzi IEBC, kuwasilisha Fomu 32As na Fomu 34 kutoka vituo 41 kama ilivyoelekezwa siku ya Jumanne.

Msajili wa mahakama alifahamisha mahakama ya juu kwamba wahusika mbalimbali hawakuweza kukubaliana jinsi ya kuendesha zoezi hilo kutokana na agizo lililotolewa kuhusu uchunguzi na kuhesabiwa kura upya Agosti 30, mwaka huu.

Pia ilielezwa kuwa mawakili wa kampuni ya (Otieno Ogola & Company Advocates) waliandikia mahakamu ya juu wakisema wanataka fomu 32 A kutoka vituo vyote 229, nao mawakili wa Njoki Mboshe waliiandikia mahakama hiyo wakitaka fomu za vituo 238 huku walalamishi nao wakiomba vituo 517, na kwamba kutokana na muda agizo hilo halitafanikiwa.

"Tunaamuru kwamba IEBC itoe Fomu 32 na 34 A Kitabu mbili kutoka kwa vituo 41 katika maombi ya celestine Anyango Apiyo, hiyo ndiyo njia pekee ambayo zoezi hilo linaweza kuwa na maana," alisema Jaji Lenaola.

Aliongeza kuwa kwenda zaidi ya vituo vilivyowekwa kutaunda kesi mpya kutokana na muda mfupi uliotolewa wa uchunguzi huo.

**MAMBO 9 YATAKAYOZINGATIWA**

Aidha, mahakama hiyo ya Juu ilisema itazingatia masuala tisa katika usikilizwaji wa kesi hiyo kabla ya uamuzi wake unaotarajiwa kutolewa Septemba 5 mwaka huu.

Majaji saba walinuia kutathmini iwapo teknolojia ya uchaguzi, iliyotumiwa hasa kufuatilia matokeo kutoka vituo vya kupigia kura hadi kituo cha kitaifa cha kuhesabia kura, ilikidhi viwango vya uadilifu, uthibitisho, usalama na uwazi.

Vile vile ilibainishwa kuwa makosa katika mfumo wa kielektroniki yalisababisha Mahakama ya Juu kufutilia mbali uchaguzi uliopita wa urais wa Agosti 2017 ambao ni wa kwanza barani Afrika, baada ya Odinga kukata rufaa.

Agosti 30 mahakama hiyo iliamuru IEBC kumpa Odinga na walalamishi wengine idhini kamili na usiozuiliwa kutazama seva za kompyuta zilizotumiwa kwa uchaguzi, huku Odinga akidai kwamba wavamizi walivamia seva na kuzipakia fomu za matokeo ya uchaguzi ya uongo, madai ambayo rais wa IEBC alikanusha.

Pia alisema kuwa matokeo katika angalau vituo 14 kati ya 46,000 yanapaswa kupitiwa na kuhesabiwa upya.

"Baada ya kutathmini uwazi wa kura hiyo, itabainisha iwapo William Ruto amefikia kiwango cha kikatiba cha asilimia 50 pamoja na kura moja kutangazwa kuchaguliwa katika duru ya kwanza," alisema.

Kwa mujibu wa RFI, tangu mwaka 2002, chaguzi zote za urais nchini Kenya zimekuwa zikipingwa, wakati mwingine kusababisha ghasia za baada ya uchaguzi na machafuko hasa ya mwaka 2007.

Wakati wa kampeni za uchaguzi, Ruto na Odinga walikuwa wameahidi kutatua tofauti zozote mahakamani badala ya mitaani.

Ikiwa Mahakama ya Juu itabatilisha uchaguzi huo, ni lazima kura mpya ifanyike ndani ya siku 60, na kwamba iwapo itathibitisha matokeo hayo, William Ruto atakuwa rais wa tano wa Kenya tangu nchi hiyo kupata uhuru mwaka 1963.

**BBC/RFI**

# JANZA ATAMBA STARS ITAWAONDOA CRANES

**Na Saada Akida**

KOCHA mpya wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Honour Janza, amesema anaamini Tanzania inaweza kupata ushindi katika mchezo wa marudiano dhidi ya Uganda na hatimaye kusonga mbele kwenye mashindano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Janza, ambaye alikuwa Kocha Mkuu wa Namungo amekabidhiwa mikoba ya kuinoa Taifa Stars akirithi nafasi iliyoachwa na Kim Poulsen.

Akizungumza na gazeti hili jana, Janza alisema anayafanyia kazi mapungufu mbalimbali aliyoyaona katika kikosi hicho baada ya kuutazama mchezo uliopita na wataingia uwanjani kurudiana na Cranes wakiwa imara zaidi.

Janza alisema, mpira wa siku hizi umebadilika na timu yoyote inaweza kupata matokeo chanya ugenini.

"Mpira hivi sasa umebadilika sana na una matokeo ya kushangaza, licha ya Tanzania kuwa nyuma kwa bao 1-0 lakini ninaamini bado timu hizi (Tanzania na Uganda) zina asilimia 50 /50 kufuzu fainali za Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wanaocheza ligi ya ndani.

"Naamini bado tuna nafasi ya kusonga mbele kama The Cranes walishinda hapa nyumbani kuna uwezekano Tanzania pia inakwenda kushinda Uganda hilo linawezekana, binafsi mimi napenda kushinda na huwa nafurahia kupata ushindi kwa sababu nimewahi kuonja ladha yake na ndio maana huwa nafurahia kupata matokeo ya kushinda" alisema Janza.

Aliongeza, kwa sasa malengo yao ni kupata ushindi katika mchezo huo na watafanya kila linalowezekana ili kupata matokeo chanya.

"Naamini tunatakiwa kuungana na kushirikiana ili kufikia malengo, katika mechi hii iliyoko mbele yetu na nyingine zitakazofuata, mimi au benchi la ufundi peke yetu hatuwezi, umoja unaleta mafanikio," Janza aliongeza.

Cranes, inayonolewa na Mserbia, Sredojovic Milutin 'Micho' itawakaribisha Taifa Stars Jumamosi kwenye Uwanja wa St Marry's Katende uliopo jijini Kampala.



Mchezaji wa All Stars Veterans, Rafiki Ntoke (kushoto), akijiandaa kumtoka nyota wa Mafather Veterans katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Jakaya Kikwete Youth Park jijini Dar es Salaam Jumapili iliyopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Makocha waitwa darasani Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SHIRIKISHO la Mpira wa Miguu Zanzibar (ZFF) linatarajia kuendesha mafunzo ya sheria 17 za mchezo huo kwa makocha wanaofundisha timu za Ligi Kuu visiwani hapa pamoja na wale wa Ligi za Kanda, imefahamika.

Mafunzo hayo yatakayofanyika leo na kesho, pia yatawahusisha manahodha wa timu zote zinazoshiriki ligi hizo.

Mkurungenzi wa Ufundi wa ZFF, Salum Ali Haji, aliliambia gazeti hili mafunzo hayo yataendeshwa na Mkufunzi wa ndani wa waamuzi, Ramadhani Ibada Kibo, na lengo lake ni kuwafahamisha kuhusu sheria zilizofanyiwa mabadiliko katika msimu huu wa 2022/2023.

Haji alisema, wanaamini mafunzo hayo yatawajengea makocha na manahodha hao uelewa mpana wa sheria za soka na hatimaye kusaidia kupokea maamuzi mbalimbali yatakayofanyika kwenye mechi wanazocheza.

"Makocha na wachezaji wamekuwa vinara wa kuwalalamikia waamuzi pale wanapofanya uamuzi wao, pengine hufanya hivi kwa kutokujua mabadiliko ya sheria au kufanya makusudi, naamini mafunzo haya yatawafungua na kumaliza malalamiko," Haji alisema.

Aliongeza kwa kuwataka washiriki kuzingatia elimu watakayopewa kwa kuyafikisha kwa timu wanazotoka ili kuleta ufanisi na mabadiliko katika kazi zao huku pia ikisaidia kumaliza dhana ya kuonewa.

## JKT Tanzania FC yaiwaza Ligi Kuu

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa JKT Tanzania umesema umejipanga kuhakikisha timu yao inarejea katika Ligi Kuu Bara msimu ujao na hilo ndio lengo kuu la kumwajiri kocha, Malale Hamsini.

Katibu Mkuu wa JKT Tanzania, Abdul Nyumba, alisema wamesajili kikosi imara kitakachosaidia kutimiza malengo yao katika Ligi ya Championship wanayoshiriki ambayo msimu mpya wa 2022/2023 utaanza ifikapo Septemba 17, mwaka huu.

Nyumba alisema wanaamini maboresho yaliyofanyika katika benchi la ufundi yatawasaidia kufikia malengo ya kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kufahamu walipokosea msimu uliopita.

Aliwataja wachezaji wapya 10 ambao wamewasajili kuongeza nguvu ni Hassan Kapalata, Emmanuel Kichiba, Ally Yusuph, Riphat Msuya, Mohammed Katoto, Maka Edward, Maulid Juma, Richard Jovit, Siraji Juma na Himid Yusuph.

"Msimu huu tumejipanga kurejea rasmi katika Ligi Kuu moja kwa moja, tumefanya usajili mzuri na kufanya Pre Season safi, hatutaki kucheza Play Off," alisema Nyumba.

Katika kujiandaa na msimu mpya, JKT Tanzania inatarajia kucheza mechi ya kirafiki dhidi ya Namungo FC leo kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

## Mieleka kufanya uchaguzi Oktoba

**Na Saada Akida**

UCHAGUZI Mkuu wa Chama cha Mieleka ya Ridhaa Tanzania (TAWF), umepangwa kufanyika ifikapo Oktoba 28, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Najaha Bakari, alisema fomu kwa ajili ya wadau wanaotaka kuwania nafasi mbalimbali zilianza kutolewa jana na mwisho wa zoezi hilo ni Oktoba 24, mwaka huu.

Bakari, alizitaja nafasi zinazowaniwa ni pamoja na Rais, Makamu Rais, Katibu Mkuu, Katibu Msaidizi, Mweka Hazina na nafasi tatu za wajumbe wa Kamati ya Utendaji.

"Ada ya fomu kwa nafasi tano za juu ni Sh. 100,000 na kwa nafasi ya ujumbe ni Sh. 50,000. Usaili wa wagombea utafanyika siku mbili kabla ya uchaguzi," alisema ofisa huyo.

Aliongeza, kwa kuwataka wadau wenye sifa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi ili chama hicho kipate safu ya viongozi iliyokamilika kwa maendeleo ya mchezo huo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NYOTA KUTUA FULHAM
FULHAM ina matumaini ya kumsajili winga wa zamani wa Brazil, Willian mwenye umri wa miaka 34, nyota wa Paris St-Germain na Ufaransa, Layvin Kurzawa (29), fowadi wa Roma na Uholanzi, Justin Kluivert (23), na mshambuliaji wa Marseille na Senegal, Bamba Dieng (22). ***(Telegraph)***

### GAKPO AGEUKA LULU
EVERTON na Leeds United wameungana na Southampton kujaribu kumsajili Cody Gakpo. Klabu yake ya PSV Eindhoven awali ilikataa ombi la euro milioni 25 mapema wiki hii kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 23. ***(Telegraph)***

### BRIGHTON YAMTAKA CAICEDO
KLABU ya Brighton imesema haitashinikizwa kumuuza kiungo wao wa kimataifa wa Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 20, ambaye amekuwa akihusishwa na uhamisho wa pauni milioni 42 kwenda Liverpool. ***(TalkSport)***

### GVARDIOL ANUKIA CHELSEA
CHELSEA wako katika mazungumzo ya kukamilisha dili la pauni milioni 77 kwa mlinzi wa Croatia, Josko Gvardiol mwenye umri wa miaka 20 kufikia tarehe ya mwisho ya uhamisho leo Alhamisi. ***(Mail)***

### WAN-BISSAKA APATA RUKSA
MANCHESTER United itamruhusu Aaron Wan-Bissaka mwenye umri wa miaka 24, kuondoka katika klabu hiyo iwapo watakubaliana kumnunua kwa mkopo Sergino Dest wa Barcelona (21), ambaye ni mchezaji wa kimataifa wa Marekani. ***(90min)***

### ARSENAL, EVERTON VITANI
ARSENAL na Everton ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomhitaji winga wa Shakhtar Donetsk ,na Timu ya Taifa ya Ukraine, Mykhaylo Mudryk mwenye umri wa miaka 21. ***(Metro)***

### PAREDES ANUKIA JUVE
KLABU ya Juventus inatarajia kukamilisha mkataba wa mkopo kumnunua kiungo wa kati wa PSG na Timu ya Taifa ya Argentina, Leandro Paredes mwenye umri wa miaka 28, ambaye alikuwa akiivutia Arsenal. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### FAES ATAJWA LEICESTER
LEICESTER City ipo katika mazungumzo juu ya mkataba wa pauni milioni 17.2 kumnunua beki wa Reims, Wout Faes mwenye umri wa miaka 24, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji akionekana kama mbadala wa mlinzi wa Ufaransa, Wesley Fofana (21), ambaye anakaribia kuhamia Chelsea kwa dau la pauni milioni 70. ***(Mail)***

### BOLY AKARIBIA FOREST
MLINZI wa Ivory Coast, Willy Boly, mwenye umri wa miaka 31, atafanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Nottingham Forest kabla ya kununuliwa kwa dau la pauni milioni 2.25 kutoka Wolverhampton Wanderers. ***(Athletic - subscription needed)***

### BELLERIN KUTUA BARCA
BARCELONA wanajipanga kumnunua beki wa kulia wa Arsenal na Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 27, ikiwa hawataweza kumpata mlinzi wa Argentina, Juan Foyth (24) kutoka Villarreal. ***(90min)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KIWANGO CHA CHELSEA CHAMTIA HOFU TUCHEL

●●● Imetokana na timu yake kupata kipigo cha pili mfululizo ugenini na...

**LONDON, England**

BAADA ya Chelsea kupokea kichapo cha mabao 2-1 katika mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Southampton, Kocha Thomas Tuchel, amesema The Blues hao lazima waimarike "haraka iwezekanavyo".

Chelsea walichukua uongozi kupitia kwa Raheem Sterling juzi Jumanne usiku, lakini mabao ya Romeo Lavia na Adam Armstrong yalibadilisha mwelekeo na wao kuchezea kichapo cha magoli 2-1.

Wakiwa wamechapwa mabao 3-0 na Leeds United katika safari yao ya mwisho ya ugenini, Chelsea sasa wamepata vipigo mfululizo vya ugenini kwa mara ya kwanza tangu Desemba, mwaka juzi.

Tuchel, kwa upande wake, amepoteza mfululizo katika Ligi Kuu England kwa mara ya kwanza tangu alipokuwa akiifundisha Paris Saint-Germain mnamo Agosti, mwaka 2019.

Baada ya mchezo huo, Tuchel alishindwa kueleza matatizo yao na kusema wanahitaji kuimarika tu.

"Sijui kama neno linahusika, sipendi kabisa kupoteza na ni mara ya pili katika msimu, mapema sana," alisema akiiamba BT Sport.

"Nadhani haihitaji sana kushinda. Hiki ndicho sipendi. Tuna unyenyekevu wa kutosha kuelewa tunaweza kupoteza mechi na bila shaka, mechi za ugenini.

"Hatupendi na tunajaribu kushinda kila mechi lakini jinsi tunavyofanya hivi ni jambo ambalo tunapaswa kuelewa haraka iwezekanavyo na kubadilika.

"Ni ngumu, sijui kwanini, tunaanza vizuri katika michezo yote karibu, na ni wazi tunapambana na umakini wetu na uthabiti katika mechi.

"Haitoshi kucheza dakika 20 vizuri, tulifanya hivyo hivyo kule Leeds. Kisha jambo moja linaenda kinyume na sisi, na tunatatizika kutafuta majibu na kupambana na njia yetu ya kurejea ikiwa mambo hayaendi katika mwelekeo wetu."

Wakati huo huo, Sterling sasa amefunga kila moja ya mabao matatu ya mwisho ya Chelsea, na wakati Tuchel ana wasiwasi na ushambuliaji wa wachezaji wake, alisisitiza umuhimu wa kugundua tena utulivu wao wa ulinzi.

"Nadhani katika dakika 20 za kwanza tulitengeneza nafasi, nusunusu lakini tulijitahidi kufunga, jambo ambalo pia si geni kwetu na si lazima kuwe na matokeo ya kupoteza mechi.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,027,3

MECHI KALI

LEICESTER
VERSUS
MANCHESTER UTD

1 | 3.10
X | 3.50
2 | 2.12

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.


tigo pesa
vodacom | m-pesa
airtel money
ZANTEL EZYPESA

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# CITY YAJIPANGA KUMSAJILI AKANJI

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester City ipo katika mazungumzo na Borussia Dortmund kwa ajili ya kumnunua, Manuel Akanji, kwa mujibu wa 90min.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uswizi amebakiwa na chini ya mwaka mmoja kukamilisha mkataba wake katika klabu hiyo ya Signal-Iduna Park na hajaonekana kwenye kikosi hadi sasa msimu huu.

Akanji amekuwa akihusishwa kuhamia Leicester na Manchester United siku za hivi karibuni, lakini 90min inaelewa mazungumzo yanaendelea kati yake na Manchester City.

Mwanzo mbaya wa John Stones hadi msimu huu na hitaji la Nathan Ake kucheza nafasi ya beki wa kushoto baada ya kuondoka kwa Oleksandr Zinchenko inamaanisha Pep Guardiola anatafuta suluhu haraka.

Dili la Akanji linatarajiwa kugharimu chini ya pauni milioni 15, jambo ambalo linamfanya kuwa chaguo la kuvutia pale City.

City wameruhusu mabao matano katika mechi zao nne za kwanza za Ligi Kuu England, rekodi ambayo sio nzuri kwao.

Akanji mwenye umri wa miaka 27 ameichezea Dortmund mechi 158 tangu ajiunge nayo kutoka Basel mwaka wa 2018.

# Saka ana imani atasaini mkataba mpya

**LONDON, England**

BUBAYO Saka ana imani atakubali kusaini mkataba mpya na Arsenal, akifichua anahisi "kupendwa sana" na Mikel Arteta na wachezaji wenzake hapo kwenye dimba la Emirates.

Saka ameibuka kama sehemu muhimu ya kikosi cha Arsenal tangu alipoanza kucheza ligi hiyo mwaka 2019, na alitikisa nyavu mara 11 na kumaliza kama mfungaji bora wa timu hiyo katika Ligi Kuu England msimu uliopita.

Tangu kuanza kwa kampeni iliyopita, hakuna mchezaji wa Arsenal ambaye ameandikisha pasi nyingi za mabao katika ligi hiyo kama Saka (nane).

Ingawa mkataba wa sasa wa Saka unamalizika mwaka 2024, Arsenal wana nia ya kumuongezea mwingine mapema ili kuepuka kuwekwa katika mazingira magumu mwishoni mwa msimu.

Kabla ya ushindi wa 3-0 dhidi ya Bournemouth mapema mwezi huu, Arteta alisema "ana uhakika sana" mkataba mpya utakubaliwa na mchezaji huyo wa kimataifa wa England.

Wakati maoni hayo yalipowekwa kwa Saka kabla ya mechi ya Ligi Kuu ya Arsenal dhidi ya Aston Villa Jumatano, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20 alijibu: "Nina imani kubwa na hilo.

"Ninahisi upendo kutoka kwa wachezaji wenzangu, makocha wangu na mashabiki pia. Ninahisi kupendwa sana hapa."



## HABARI MICHEZO

393,141/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/09/22 | 17:00 | Swansea City vs Queens Park Rangers | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 02. 03/09/22 | 17:00 | Rotherham United vs Watford FC | 2.90 | 3.15 | 2.41 |
| 03. 03/09/22 | 19:00 | AC Milan vs Inter Milano | 2.60 | 3.25 | 2.60 |
| 04. 03/09/22 | 19:00 | FC Sion vs FC Basel 1893 | 2.60 | 3.30 | 2.50 |
| 05. 03/09/22 | 19:30 | Real Sociedad San Sebastian vs Atletico Madrid | 2.80 | 3.10 | 2.50 |
| 06. 03/09/22 | 19:30 | SD Ponferradina vs Sporting Gijon | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 07. 03/09/22 | 20:00 | AC Omonia Nicosia vs AEK Larnaca | 2.50 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 03/09/22 | 21:45 | Lazio Rome vs SSC Napoli | 2.80 | 3.35 | 2.36 |
| 09. 04/09/22 | 02:00 | New York Red Bulls vs Philadelphia Union | 2.35 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 04/09/22 | 14:00 | Reading FC vs Stoke City | 2.85 | 3.15 | 2.43 |
| 11. 04/09/22 | 14:30 | Hansa Rostock vs Hannover 96 | 2.49 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 04/09/22 | 15:00 | Odense Boldklub vs Viborg FF | 2.55 | 3.50 | 2.48 |
| 13. 04/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs FC Lorient | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 14. 04/09/22 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Strasbourg Alsace | 2.90 | 3.40 | 2.28 |
| 15. 04/09/22 | 17:00 | Huddersfield Town vs Blackpool | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 16. 04/09/22 | 18:30 | Manchester United vs Arsenal FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 04/09/22 | 21:30 | Aris Thessaloniki vs PAOK Thessaloniki | 2.39 | 3.15 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 01/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 2363 | Shijiazhuang vs Shanghai SIPG | 5.87 | 3.82 | 1.50 |
| 14:30 | 2594 | Hangzhou NG vs Guangzhou Evergrande | 1.30 | 4.61 | 8.63 |
| 14:30 | 3280 | Changchun Yatai vs Chengdu Qianbao | 2.03 | 3.35 | 3.25 |
| 14:30 | 4505 | Sabah vs Kuala Lumpur | 1.72 | 3.58 | 4.21 |
| 14:30 | 4625 | Dalian Aerbing vs Shenzhen | 1.62 | 3.69 | 4.72 |
| 16:00 | 2325 | Kabwe Warriors vs Red Arrows | 3.09 | 2.50 | 2.65 |
| 16:00 | 5754 | Torpedo Kutaisi vs FC Samgurali Tskaltubo | 3.03 | 3.23 | 2.17 |
| 16:00 | 5843 | Sioni Bolnisi vs FC Gagra | 2.31 | 3.29 | 2.75 |
| 16:30 | 2916 | Rigas Futbola Skola vs SC Grobina | 1.04 | 11.81 | 17.71 |
| 16:45 | 2507 | Sohar Club vs AL Etihad | 1.95 | 3.05 | 3.88 |
| 17:00 | 5510 | Queretaro U20 vs Puebla U20 | 2.85 | 3.64 | 2.11 |
| 17:30 | 2605 | Lechia Dzierzoniow vs GKS Piast Gliwice | 21.68 | 12.81 | 1.02 |
| 18:00 | 3542 | Haka vs Honka | 3.14 | 3.24 | 2.11 |
| 18:00 | 4430 | Botosani vs Argesul Pitesti | 2.04 | 3.20 | 3.60 |
| 18:00 | 4895 | Taby FK vs Norrkoping | 14.82 | 12.85 | 1.05 |
| 18:30 | 1437 | SV Allerheiligen vs Rapid Vienna | 14.78 | 8.47 | 1.09 |
| 18:40 | 2876 | AL Sahel vs AL Nasr | 3.00 | 3.49 | 2.08 |
| 19:00 | 1784 | Ramtha Club vs AL Salt | 2.23 | 2.95 | 3.20 |
| 19:00 | 2335 | Cukaricki St vs Mladost Lucani | 1.45 | 4.13 | 5.89 |
| 19:00 | 2835 | OKS Odra Opole vs Jagiellonia | 3.92 | 3.38 | 1.82 |
| 19:00 | 2950 | Oman Club vs Rustaq Club | 2.80 | 2.80 | 2.60 |
| 19:00 | 4069 | FK Auda vs Jelgava | 1.51 | 3.95 | 6.00 |
| 19:00 | 4193 | Hvidovre IF vs Hobro | 1.57 | 3.83 | 4.92 |
| 19:00 | 4867 | Viimsi JK vs Parnu Jalgpalliklubi | 1.35 | 5.24 | 7.25 |
| 19:00 | 5692 | Harju JK Laagri vs FCI Levadia Tallinn U21 | 2.10 | 3.80 | 3.04 |
| 19:30 | 4521 | Vidar vs Brodd | 1.82 | 4.32 | 3.14 |
| 19:45 | 5531 | Mar de Fondo FC vs CS Cerrito | 4.91 | 3.58 | 1.62 |
| 20:00 | 1799 | El Fahem vs SC Kfar Qasem | 2.44 | 3.15 | 2.85 |
| 20:00 | 2222 | Vastra Frolunda IF vs Utsiktens BK | 7.26 | 6.28 | 1.25 |
| 20:00 | 2709 | Ironi Hasharon vs Maccabi Petach Tikva | 3.47 | 3.32 | 2.08 |
| 20:00 | 2910 | Sandvikens IF vs Sirius FK | 6.26 | 5.29 | 1.33 |
| 20:00 | 3178 | Nazareth Ilit vs Hapoel Acre | 1.87 | 3.15 | 4.50 |
| 20:00 | 3379 | Budapest Honved vs Ujpest FC | 2.31 | 3.38 | 2.69 |
| 20:00 | 4071 | Dinamo Tbilisi vs Loko Tbilisi | 1.09 | 11.00 | 14.00 |
| 20:00 | 4457 | Dinamo Batum vs FC Telavi | 1.22 | 6.00 | 11.00 |
| 20:00 | 5516 | Ahi Nazareth vs Ironi Tiberias | 2.46 | 3.17 | 2.87 |
| 20:00 | 5589 | Hapoel Ramat Gan vs Bnei Yehuda | 2.41 | 3.08 | 3.03 |
| 20:25 | 2429 | Arka Gdynia vs Gornik Leczna | 1.78 | 3.44 | 4.03 |
| 20:30 | 3008 | KI Klaksvik vs B36 Torshavn | 1.21 | 6.12 | 8.88 |
| 21:00 | 2399 | Telstar vs De Graafschap | 3.42 | 3.62 | 1.93 |
| 21:00 | 2450 | AZ Alkmaar vs NEC Nijmegen | 1.46 | 4.40 | 5.99 |
| 21:00 | 2907 | Abha vs Al Shabab Riyadh | 5.25 | 4.03 | 1.58 |
| 21:00 | 2967 | AL Tadamon vs Al Kuwait SC | 5.12 | 4.14 | 1.51 |
| 21:00 | 3237 | Hermanstadt vs Universitatea Craiova | 3.85 | 3.15 | 1.99 |
| 21:30 | 2538 | Ruch Chorzow vs Gornik Zabrze | 3.63 | 3.29 | 1.92 |
| 21:30 | 5971 | Anderlecht vs KAA Gent | 2.17 | 3.47 | 3.07 |
| 21:45 | 3628 | Bologna vs Salernitana | 1.83 | 3.55 | 3.95 |
| 21:45 | 5315 | Atalanta vs Torino | 1.66 | 3.85 | 4.60 |
| 22:00 | 5807 | JS Kabylie vs CS Constantine | 1.91 | 3.04 | 4.02 |
| 22:00 | 5978 | Leicester vs Manchester Utd | 3.10 | 3.50 | 2.12 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SPORTPESA KINARA KATIKA UBORA WA HUDUMA ZAKE

**Na Mwandishi Wetu**

KAMA mnavyojua msimu wa ligi karibu zote duniani ndio hivyo unayoyoma na kwa sasa ligi ya nyumbani imesimama kupisha michezo ya kimataifa ambayo timu za taifa ikiwamo ya kwetu Tanzania zinapambania kufuzu kucheza makombe mbalimbali yanayoratibiwa na CAF, kama CHAN na mengineyo.

Meneja Uhusiano na Mawasilaino wa Sportpesa, Sabrina Msuya, alisema kwao Sportpesa huduma ya kubashiri inaendelea kama kawaida ambapo kwa sasa kuna Jackpot ya katikati ya wiki na Jackpot ya mwisho wa wiki inayofahamika kama Supa Jackpot.

Alisema, Jackpot za Sportpesa zimeboreshwa ili kumpa mchezaji wigo mpana wa kuweza kushinda na kufurahia thamani ya pesa anayotumia ama kucheza na SportPesa.

"Kwanza kabisa Supa jackpot inaanzia bilioni moja ambapo sasa hivi ni 1,025,118,259 TZS, Pili ukuachia jackpot ya mechi 17, chini yake kuna Jackpot ya mechi 16, 15, 14 na 13. Jackpot zote hizi mteja wetu anaweza jishindia vitita vinono vya pesa kupitia bonus ambazo zinapatikana iwapo mteja atakuwa amekosa baadhi ya mechi.

"Kampuni yetu imejitahidi kutoa huduma ambayo inalenga kumkomboa ama kumuwezesha mtanzania kutimiza ndoto zake. Ukiangalia tangu tumeanza mpaka hivi sasa utagundua Sportpesa imeweka bidhaa na huduma ambazo ni rahisi kufikika na pia kutumika."

Anaendelea kusema kuwa moja ya bidhaa ambayo Sportpesa ilileta ni kubashiri kwa kutumia USSD na SMS ambapo mchezaji mwenye simu ya kitochi maarufu kama kiswaswadu anacheza bila shinda na tena bila kukatwa hata senti moja. Pia wachezaji wa simu za Android na IOS wanacheza bila kuwa na bando.



Meneja Uhusiano na Mawasilaino wa Sportpesa, Sabrina Msuya, akizungumzia namna kampuni yao ya huduma ya kubashiri inavyotoa huduma zenye ubora mkubwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Hili ni eneo mojawapo ambapo tumekuwezesha mteja na kukupa fursa ili uweze kujaribu bahati yako, bila mkwamo wa aina yoyote. "Kama wewe ni mfuatiliaji utagundua huduma zetu zimelenga watu wa rika na vipato vyote".

Katika kuboresha huduma zetu tuliamua kuwekeza zaidi kwenye teknolojia na mifumo ya tehama ambayo hii inawapa urahisi wateja wetu katika kufurahia huduma na bidhaa zetu. Hapa natolea mfano mteja wetu sasa anaweza kutatuliwa matatizo au changamoto muda wowote katika masaa 24.

Kwa wale ambao wanapenda kubashiri lakini hawana muda kutokana na aina ya majukumu na nafasi zao katika jamii hatukuwaacha mbali. Kwa kutumia mitandao ya Facebook, Twitter na WhatsApp tumewawekea huduma ya "Share Mkeka" ambapo unaweza kutengeneza mkeka na ukamtumia ndugu jamaa na rafiki yako naye akaweka kwa kuweka kiasi anachotaka au kuhariri kidogo na kuweka ubashiri.

Ukiangalia aina ya washindi ambao wamekuwa wakipatikana kupitia bidhaa zetu, utagundua tuna rika zote ambazo zinaruhusiwa kisheria kushiriki michezo hii ya kubashiri. Karibu kila siku washindi wa viwango mbali mbali wanajishindia zawadi mbali mbali za kifedha kama vile kasino, Tenisi, Jackpoti bonasi na Multibet bonasi, kwa uchache tu.

"Kwa sasa tuna michezo kama "Lucky Number" au Namba za bahati, tuna mchezo wa Virtual games, michezo ya kasino kama Hot Hot Fruit, 9 Masks of Fire, Boom Pirates na Multifire Roulette

Kwa kumalizia, Sabrina anasema watanzania wachukue fursa inayopatikana Sportpesa kwani malipo ni fasta kuliko kampuni nyingine yoyote. "Ninawaasa ndugu zangu watanzania kuendelea kucheza na Sportpesa kwa wale ambao wanacheza na kwa wale ambao hawajajiunga na sisi basi wasisite kujisajili na kucheza".

# Ruvu yaipigia hesabu Namungo

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Ruvu Shooting umesema umeamua kufuta mapumziko ya wachezaji wake kwa ajili ya kutoa nafasi kwa benchi la ufundi kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika mechi mbili zilizopita za Ligi Kuu Tanzania Bara na hatimaye kuwakabili Namungo FC wakiwa imara.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Mbwire alisema tangu kumalizika kwa mechi yao dhidi ya Mtibwa Sugar hapo Agosti 21, mwaka huu ambapo walichapwa mabao 2-1, hawakutoa mapumziko kwa wachezaji wao kama timu nyingine zilivyofanya ili kujiwinda na mchezo unaofuata.

"Tumepata maandalizi ya muda mrefu kwa sababu hatukumpumzisha mtu tangu tulipomaliza mechi ya pili, makocha wamekuwa na kazi ya kurekebisha mapungufu yaliyoonekana katika michezo miwili, wawajenge kiuwezo zaidi, ili mchezo dhidi ya Namungo tupate matokeo chanya.

Tunakwenda kucheza na Namungo, moja ya timu ambazo ziko vizuri, benchi lao lipo sawasawa japo nasikia kocha wao Hanour Janza amechukuliwa na Taifa Stars, hata usajili wao ni mzuri una wachezaji bora wa ndani na nje ya nchi," alisema Masau.

Ruvu Shooting bado itakuwa inacheza ugenini, kwa sababu ilianza msimu mpya kwa kuwafuata Ihefu kwenye Uwanja wa Highlands Estate na kushinda bao 1-0 halafu ilielekea Manungo Complex.

# Michezo

Alhamisi Septemba 1, 2022
Nipashe



## Kiwango cha Chelsea chamtia hofu Tuchel



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), wakifanya mazoezi kujiandaa kwa mechi ya marudiano dhidi ya Uganda kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN) itakayochezwa Jumamosi jijini Kampala. **PICHA: TFF**

# JOTO LA NAMBA LATIKISA SIMBA

## ...Kocha aeleza bado ana kibarua cha kukisuka kikosi chake huku ushindani...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jana usiku ilishuka dimbani kucheza mechi yake ya mwisho ya mashindano maalumu huko Sudan dhidi ya wenyeji, Al Hilal, Kocha Mkuu wa Simba, Zoran Maki, bado amekuwa na maingizo tofauti katika kikosi chake cha kwanza cha Wekundu hao wa Msimbazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema wachezaji wa timu hiyo wamekuwa na ushindani mazoezini na katika mechi zote walizocheza kwa sababu hakuna ambaye anaamini amepata namba ya kudumu.

Matola alisema kupata michezo mingi ya kirafiki pia kumesaidia kuwaimarisha wachezaji wao kwa sababu wanakabiliwa na mechi ngumu za Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanayokwenda kushiriki.

"Bado tunasuka kikosi, tumekuwa tukiwatumia wachezaji tuliokuwa nao hapa katika michezo hii kwa maana ya kuwaimarisha zaidi, ninaamini baada ya mashindano haya mwalimu (Maki), atakuwa amepata kikosi chake," alisema Matola.

Aliongeza kuna wachezaji ambao msimu uliopita walionekana wamejihakikishia namba lakini kwa sasa hali imebadilika, hivyo mabadiliko haya yanawafanya nyota wetu kuendelea kujituma zaidi.

"Mechi hizi zimetusaidia kuelekea mechi yetu ya kimataifa dhidi ya Big Bullet ya Malawi, zimetupa nafasi ya kuwaangalia wachezaji ambao hawakupata nafasi, tumewaangalia wachezaji wengine ambao hawakupata nafasi na kupata picha halisi ya timu nzima," Matola alisema.

Aliongeza wakati wanaendelea na michezo hiyo, benchi la ufundi limeendelea kuwafuatilia wapinzani wao, Big Bullet ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kuvuna matokeo chanya.

"Siku hizi hakuna timu ndogo, tutaenda Malawi kuwakabili wapinzani wetu kwa tahadhari zote, hatutaki kuwa na mlima mkubwa tutawapowaalika katika mechi ya marudiano nyumbani, tumejipanga kufika mbali," Matola alisema.

Wakati huo huo, kiungo, Sadio Kanoute, raia wa Mali na nahodha, John Bocco walijiunga na timu hiyo iliyoko Sudan tangu juzi na kukiongezea nguvu kikosi chao.

"Ujio wa Kanoute na Bocco ni faraja kwetu, kunaendelea kumpa wigo kocha na hatimaye baada ya kumaliza mechi hizi, tutakuwa na mwanga wa wapi tutakwenda," aliongeza kocha na nahodha huyo wa zamani wa Simba.

Katika hatua nyingine, Kanoute, Pape Sakho na Clatous Chama wametajwa kuwania tuzo ya mchezaji bora wa Agosti wa Simba.

Hata hivyo, rekodi zinampa nafasi kubwa ya Chama ambaye amecheza mechi mbili za ligi na kufunga bao moja na kutoa pasi moja ya bao kwenye mchezo dhidi ya Kagera Sugar kushinda tuzo hiyo inayodhaminiwa na Kampuni ya Emirate Aluminium.

## Yanga, Azam FC zinasubiri muda

**Na Mwandishi Wetu**

MABOSI wa timu za Yanga na Azam FC wametamba kila kikosi kiko tayari kwa mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Septemba 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Yanga itashuka katika mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika mchezo wake wa kwanza huku pia ikiwachapa Coastal Union mabao 2-0, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nassredine Nabi, alisema anafahamu mechi hiyo itakuwa ngumu na yenye ushindani kwa sababu Azam FC pia imesajili wachezaji wazuri na wenye uzoefu.

Nabi alisema mabadiliko ya benchi la ufundi ni sababu nyingine itakayowafanya wasifahamu vyema aina ya mfumo ambao wataingia nao wapinzani wao.

"Mchezo hautakuwa rahisi, ni mchezo muhimu kwetu kupata matokeo, tutaingia tofauti, hatutatumia mbinu ambazo tulizitumia katika mechi zetu za ugenini, tutabadilisha mfumo kwa sababu kila mchezo unahitaji mpango kazi tofauti," alisema Nabi.

Naye Mkurungenzi wa Mashindano wa Yanga, Saad Kawemba, alisema kikosi chao kiliendelea kujiimarisha kwa kufanya mazoezi magumu kwa sababu hawakupata muda wa kutosha wakati wa Pre Season.

Aliongeza mechi za kirafiki ambazo wamecheza wakati ligi imesimama zilikuwa na malengo ya kiufundi na si kuangalia matokeo ya mwisho kama inavyotafsiriwa.

Naye Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zakaria, alisema kikosi chao kinaendelea kuimarika na hawana hofu yoyote kuelekea mechi yao dhidi ya Yanga.

"Tunasubiri muda, mazoezi yanayoendelea ni ya kuiweka miili ya wachezaji wetu tayari, lakini kiufundi tulishamaliza kazi," Zaka alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042